
# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | T anuari 29, 2022 NAKALA BILA MALIPO


# MAMBO BADO

**Kiongozi wa Azimio la Umoja-One Kenya anaonya kuwa kama Uchaguzi Mkuu wa 2022 'hautachunguzwa na kumalizwa vizuri', Wakenya wanafaa 'kusahau kuhusu uchaguzi mwingine wa urais 2027'**

# The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe
> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation
Nation
Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

# Yaliyomo

**9 KISIMA CHA KUCHOTA PESA CHAKAUKA:** Mkataba wa muda mrefu wa kuchapisha pesa kati ya kampuni ya Uingereza, De La Rue, na serikali ya Kenya unaonekana kufikia mwisho.

**10 MISIMAMO YABADILIKA:** Rais Ruto anaendelea kupenya ngome ya Jubilee huku wanasiasa walioshindwa kwenye uchaguzi eneo la Mlima Kenya na maeneo mengine nchini wakihamia polepole chama tawala.

**22 INJERA AONDOKA ULINGONI:** Mchezaji huyo mkongwe ameacha mchezo wa raga baada kushirika mashindano 279 ya wachezaji Saba kila upande, mechi nne za Kombe la Dunia, kucheza mara 424 katika mashindano 83 ya kimataifa - nyingi zaidi kuwahi kucheza na Mkenya - na mashindano mawili ya Olimpiki.

**25 CHUMA CHA ZUMA MOTONI:** Bila mabadiliko katika mwelekeo wake wa sasa, aliyekuwa rais na mfungwa mara mbili huenda akatupwa gerezani tena.



*- Zimetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Baada ya uchaguzi, huu ni wakati wa kuanza kuponya taifa lililogawanyika

Chaguzi huja na kuisha, linasema wazo la kidemokrasia. Pia kuna msemo wa Kikristo kwamba kuna wakati wa kila kitu duniani – wakati wa kupanda na wakati wa kuvuna, wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa.

Ni rahisi kukubali haya yote kuwa hekima kama mtu hajui chochote au anajua machache zaidi kuhusu siasa za Kenya.

Hapa, chaguzi huwa haziishi; kampeni huendelea, na kushika kasi kwa kelele za juu; na uhasama wa kuudhi wa kisiasa huendelea kwa muhula wote hadi uchaguzi mwingine utakapofanywa, miaka mitano baadaye.

Inaonekana kwamba ili wanasiasa wetu waendelee kuzungumziwa, ni lazima wasababishe migongano nchini. Ili kudumisha uaminifu wa waliowaunga mkono katika uchaguzi, ni lazima waingize ajenda za kuleta migawanyiko katika kila kitu kinachounganisha taifa.

Ushindani katika uchaguzi wa Agosti 9 ulikuwa wa karibu sana, na hivyo, upande mmoja wa nchi uliachwa ukisherehekea ilhali upande mwingine ulikuwa ukichemka kwa hasira.

Watu wa maeneo fulani, na makabila, wanaonekana kuwa na ajenda tofauti. Huku wengine wakiitakia serikali ufanisi, wengine wanaomba usiku na mchana kwamba utawala huu uporomoke ili kuthibitisha kuwa matamanio yao ni sahihi.

Wakati huu, ni rahisi kwa walio katika upinzani kulaumu utawala huu mpya kwa kila kitu kinachoenda vibaya, wakisema 'Si nilikwambia.'

Ni kweli kwamba karibu nusu ya watu bado wana hasira na wanahisi kura ziliibiwa ilhali nusu ya wengine wanasifu kila kitu, hata sera ambazo hivi karibuni huenda zikatudhuru. Mgawanyiko huu ni hatari kwa umoja wetu wa kitaifa na lazima liwe suala la kwanza kwetu kushughulikia, ili kuwe na uwiano tunaohitaji zaidi.



**Allan Buluku**

**Ni kweli kuwa karibu nusu ya watu bado wana hasira na wanahisi kura ziliibiwa ihali wengine nusu wanasifu kila kitu, hata sera ambazo hivi karibuni huenda zikatudhuru. Mgawanyiko huu ni hatari kwa umoja wetu wa kitaifa na lazima liwe suala la kwanza kwetu kushughulikia, ili kuwe na uwiano tunaohitaji zaidi.**

Alivyosema Abrahamu Lincoln, 'nyumba iliyogawanyika haiwezi kusimama'; hii ndiyo kauli mbiu tunayopaswa kukumbatia na kuwahubiria Wakenya.

Kiongozi wa Azimio la Umoja-One Kenya Raila Odinga anaamini kuwa alishinda uchaguzi, ilhali Mahakama ya Upeo iliamua tofauti. Pia ameulaumu utawala wa Kenya Kwanza kwa kujitwika wajibu wa kuunda upya Tume Huru ya Uchaguzi. Jukwaa limeandaliwa kwa awamu nyingine ya makabiliano kati ya utawala wa Ruto na Upinzani.

Ni jambo la busara kwa pande zote kufanya kazi pamoja katika kuunda upya tume ya uchaguzi. Ni kitu muhimu kufanya kwa taifa letu. Kwa hivyo, tunamshukuru Rais William Ruto kwa ziara yake majuzi eneo la Nyanza, ambalo kwa muda mrefu limekuwa ngome ya siasa za upinzani Kenya na nyumbani kwa Odinga.

Ziara hiyo ilipangwa bila dalili za utovu wa heshima kwa kiongozi huyo mkongwe. Lazima tuwapongeze viongozi wa upinzani waliochaguliwa na watu wa Nyanza kwa kumkaribisha Rais kwa furaha, upole na heshima na zawadi alizopewa kando na miradi ya maendeleo iliyokubaliwa.

Hii ilikuwa hatua kubwa katika mchakato wa kuleta uponyaji wa kitaifa na wananchi kumkubali Rais wao mpya. Ni dalili za mambo mazuri na tunataraji kwamba hivi karibuni Rais atafanya hivyo katika kaunti zingine. Kenya ni mfano mzuri wa demokrasia na amani katika eneo hili na lazima iendelee kuongoza kwa heshima.

Tunatarajia kuwa hatua hiyo ya Rais ni mwanzo wa kuleta pamoja taifa letu lililopasuka.

***abuluku@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Darubini Ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Rais alitia sahihi Mswada wa IEBC

## Ruto kutangaza jopokazi la IEBC

Rais William Ruto wiki hii anatarajiwa kutoa rasmi majina ya wanachama saba wa jopokazi la kuteua mwenyekiti na makamishna sita wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Hiyo ni baada ya Rais kutia saini kuwa sheria Mswada (Marekebisho) wa IEBC 2022 wiki iliyopita baada ya kupitishwa na Bunge.

Sheria hiyo inapendekeza kupanuliwa kwa jopokazi hilo ili kujumuisha nyadhifa mbili za Tume ya Huduma za Bunge, sawa na Baraza Kuu la Madhehebu ya Kidini Nchini, nafasi moja kwa Tume ya Huduma za Umma na nyadhifa mbili kwa Kamati ya Muungano wa Vyama vya Kisiasa na Chama cha Wanasheria Kenya.

Kubuniwa kwa jopokazi hilo kutatoa nafasi kuteua makamishna wapya.

Mwenyekiti Wafula Chebukati, Profesa Abdi Guliye na Boya Molu waliondoka baada ya muhula wao wa miaka sita.


Makamishna wengine watatu – Juliana Cherera, Justus Nyang'aya na Francis Wanderi – walijiuzulu baada ya kusimamishwa kazi na Rais Ruto.

Walipinga matokeo ya urais yaliyotangazwa na Chebukati. Kamishna Irene Masit amepinga uamuzi wa kumtimua mbele ya jopokazi linaloongozwa na Jaji Aggrey Muchelule.




Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka Wafula Chebukati (katikati) akiwa na Naibu Mwenyekiti Juliana Cherera (kushoto) na Kamishna Profesa Abdi Yakub Guliye katika Bomas of Kenya mnamo Agosti 5, 2022.

■ Ni bora kushinda kemikali ya kuiendesha




Mfano wa mfumo wa sayari. Nasa inashirikiana na tawi la utafiti la Idara ya Ulinzi ya Amerika kuunda roketi ya kutumia nguvu ya kinuklia katika maandalizi ya kutuma wanaanga katika sayari Mars.

## Roketi ya nguvu za kinuklia kusafiri Mars

Nasa inashirikiana na shirika la utafiti la Pentagon kuunda injini ya roketi inayoendeshwa kwa nguvu za kinuklia kwa maandalizi ya kutuma wanaanga kuzuru sayari ya Mars. Msimamizi wa Nasa Bill Nelson alisema Jumanne kuwa shirika hilo la masuala ya anga Amerika litaungana na Shirika la Miradi ya Utafiti wa Hali ya Juu Kuhusu Ulinzi (DARPA) "kuunda na kuonyesha teknolojia ya hali ya juu ya usafirishaji kwa kutumia kawi ya nuklia kufikia 2027."

"Kupitia teknolojia hii, wanaanga huenda wakasafiri angani na kurudi kwa kasi zaidi - uwezo mkuu wa kuandaa safari za watu katika Mars," akasema Nelson katika taarifa. DARPA ni tawi la utafiti na maendeleo la Wizara ya Ulinzi ya Amerika na limechangia katika miradi kadhaa ya uvumbuzi karne ya 20 ikiwemo intaneti. Nasa ilisema roketi zinazotumia nguvu za nuklia zinaweza kuwa bora mara tatu au zaidi kushinda kemikali ya kawaida na hatua hiyo itapunguza muda wa safari ya Mars.

Katika injini inayotumia nuklia, mtambo mahsusi hutumika kutoa viwango vya juu vya joto. Joto kutoka mtambo huo huhamishwa kwa kifaa kioevu na kugeuzwa kuwa gesi, inayofura kupitia kwa mfereji na kutoa msukumo.

■ Wataelewa zaidi maana ya demokrasia

## Wabunge kwenda semina siku nne



Wabunge wiki hii watashiriki semina ya siku nne inayonuiwa kuimarisha ujuzi wao kuhusu utendakazi bora wa Bunge na kuendeleza maadili na mitazamo ya kitaifa.

Semina hiyo, iliyoandaliwa na Bunge la Kitaifa likishirikiana na Chama cha Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA), itafanywa kati ya Januari 30 na Februari 3. Vikao hivyo vitawapa wabunge nafasi ya kuelewa shughuli za Bunge la Amerika hasa kuhusu masuala ya mabunge mawili na demokrasia ya vyama vingi.

Hiyo ni pamoja na kuwapa wabunge nafasi ya kuelewa vyema zaidi kuhusu mifumo ya bunge.

■ Alimaliza kwa mikwaju mitatu kupata ushindi

## Henderson ashinda Ubingwa wa LPGA



Brooke Henderson alilenga mara mbili masafa ya 70 kabla ya kutwaa ushindi katika Mashindano ya Ufunguzi ya gofu ya LPGA jijini Florida. Raia huyo wa Canada wa miaka 25, aliyeingia awamu ya mwisho akiongoza kwa mikwaju mitatu, alidumisha utulivu wake na kuhakikisha ushindi wake wa 13 katika LPGA kwa mtindo wa kufana.

Henderson alilipua vishimo viwili kufikia chini ya 15 kwa jumla kisha kishimo cha futi 10 kwenye kipimo cha15 kabla ya kulenga shabaha ya nne ya kuongoza kwenye kina cha 16. Alimalizia kwa kulenga ndipo mara tatu na kunyakua taji katika shindano lake la kwanza tangu ushindi Julai iliyopita katika shindano la Mabingwa la Evian.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

■ ANAWEZA KUWEKA PRESHA KUPITIA MIKUTANO, MAASI NA MAANDAMANO

# RAILA: TULISHINDA KWA HAKI NA UKWELI

**Ameridhika kwa upole kwamba ameikera serikali ya Ruto, inayoonekana kuweka kando shughuli zingine kujibu anachopanga. Lakini bado kuna maswali magumu**

• Na MACHARIA GAITHO

Tofauti na mwanasiasa mwenye hasira anayesimama katika jukwaa hadharani na kudai kwa mara nne mfululizo kuwa alipokonywa ushindi katika uchaguzi wa urais, kiongozi wa Azimio la Umoja-One Kenya Raila Odinga ni mpole, mtulivu na mwenye furaha anapakaribisha Darubuni ya Wiki afisini mwake Jumba la Capitol Hill.

Anaonekana mwembamba kuliko kawaida, amevalia shati la hariri, long'i inayomtosha vizuri na miguuni kuvaa vitatu vya aina ya "canvass loafers" rangi ya bluu. Raila katika mkutano wa faragha ni tofauti na 'simba wa kisiasa' katika mkutano wa hadhara. Ni mkarimu na mwenye kujali maslahi ya mgeni wake huku akionyesha ungwana kwa kuzima sauti ya simu yake, inayopigwa kila mara.

Nilikuwa na woga kidogo kukutana naye siku moja tu baada ya kuandika makala katika "Daily Nation" toleo la Jumanne, nikipuuzilia mbali madai ya Raila kwamba ushahidi mpya kutoka kwa mfichuzi umethibitisha kuwa alipokonywa ushindi katika uchaguzi mkuu wa 2022.

Hanikemei, halalamiki, hazungumzii hata kidogo niliyoyaandika katika makala hayo, yaliyomponda. Badala yake yuko makini kufafanua kuhusu madai kuwa mfichuzi alitoa ushahidi wa kutosha kutoka kwa "sava" za Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kuwa alishinda uchaguzi wa urais kwa kura 8.1 milioni (asilimia 57) dhidi ya kura 5.9 milioni (asilimia 41) za Rais Ruto.

Siku mbili tu baada ya mkutano mkubwa wa kisiasa katika uwanja wa kihistoria wa Kamukunji, unaoashiria maasi ya kisiasa, ambako alianzisha kampeni ya kushinikiza ukaguzi wa kura za urais zifanywe na kuwa Azimio haimtambui Ruto kama Rais, Raila anaonekana mwenye nguvu. Anajiandaa kurudi barabarani kuongoza maasi, na inaibuka kuwa maandalizi ya msururu wa mikutano kote nchini tayari yanafanywa kushinikiza uchaguzi wa 2022 uchunguzwe upya.



Kiongozi wa Azimio la Umoja Raila Odinga

Ameridhika, kwamba ameikera serikali ya Ruto, inayoonekana kuweka kando shughuli zingine kujibu anachopanga.

Lakini bado kuna maswali magumu. Mahakama ya Upeo ilitupa kesi ya Raila ya kupinga ushindi wa Rais Ruto, hivyo kuzima nafasi kwa mchakato mwingine wa kimahakama kuhusu suala hilo. Matakwa ya Raila kuwa uchaguzi ufanyiwe uchuguzi na "sava" za IEBC zifunguliwe, hatua ambayo anashikilia inaweza kufichua ukweli, yanaweza kupuuzwa. Anaweza kuweka presha kupitia mikutano ya kisiasa, maasi na maandamano barabarani, lakini kwa hatari kwamba ghasia na maafa yanaweza kutokea na ndiye atalaumiwa.

Mkakati wa Raila wa hivi punde pia umezua malalamiko kupitia madai kuwa ni mtu anayeshindwa katika uchaguzi kila mara kisha anaibua fujo ili aitwe kwa mkataba wa amani ambao utamwezesha kuingia serikalini. Anapuuzilia mbali madai hayo na bado anakabiliwa na kibarua cha kuthibitisha madai ya mfichuzi. Jibu lake ni kuwa kufunguliwa kwa 'sava' za IEBC ndiko kutatoa ukweli kuhusu jinsi, udanganyifu ulivyofanywa katika uchaguzi wa urais.

Anashindwa kujibu moja kwa moja swali kuhusu ni kwa nini hawezi kutoa nakala za fomu za matokeo ambazo zilipaswa kuwa zilikusanywa na maajenti wake katika vituo 46, 000 vya kupigia kura na fomu za hesabu za kura kutoka vituo vya kujumuisha kura katika maeneo bunge 290.

Kabla ya kukagua yaliyo katika 'sava' za IEBC na kutoa madai kuwa aliyekuwa mwenyekiti wa tume hiyo, Wafula Chebukati alimchezea karata mbaya katika kituo cha kitaifa cha kujumuisha kura katika Bomas of Kenya, fomu hizo zitatoa ithibati kuhusu iwapo hesabu za kura zilizowekwa kwenye mtandao wa IEBC kweli zilivurugwa.

Ninapomsukuma zaidi kuhusu hilo, Raila anakubali haingewezekana kwa Azimio ku-

Endelea Uk 6

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

HALI YA BAADAYE NI MBAYA, HUU SIWAKATI WA KUZUNGUMZIA KUSTAAFU

# 'SIENDI POPOTE...SITASTAAFU

## Nataka historia inikumbuke kama mtu aliyepigana na kutoa maisha yake kuhakikisha uchaguzi unaonyesha uamuzi wa watu, anasema kinara wa ODM



Kiongozi wa muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya Raila Odinga akihutubia wafuasi wake katika mtaa wa Donholm, Nairobi, mnamo Agosti 21 mwaka uliopita. SILA KIPLAGAT I NATION

**DW: Ulikuwa na mkutano wa hadhara katika Kamukunji Jumatatu iliyopita na ukaorodhesha matakwa yako baada ya ushahidi wa mfichuzi kuhusu madai ya wizi wa kura. Hata kama ukaguzi kuhusu uchaguzi utakusaidia kuthibitisha madai yako, unatarajia nini kuendelea mbele ikizingatiwa kwamba uamuzi wa Mahakama ya Upeo ulikuwa wa mwisho katika mchakato wa uchaguzi?**

**Raila:** Siongozwi na ubinafsi. Sisemi au kufanya haya kwa ajili ya Raila Odinga, lakini kwa nchi. Kila kizazi cha watu wetu kina jukumu la kuhakikisha kinafanya utawala wa nchi yetu kuwa wenye uwazi na kuwajibika kwa watu. Tumepitia awamu tofauti za maendeleo ya kitaifa. Kile ambacho hatutaki kuona ni hali ambayo nchi yetu inarudi katika enzi za giza tulizotoka. Sitaki kukumbukwa katika historia kama mtu anayekataa kukubali uamuzi wa watu, matokeo ya kura zinazopigwa na watu kwenye debe. Nataka kukumbukwa katika historia kama mtu aliyepigania na kutoa maisha yake kuhakikisha kwamba uchaguzi unaonyesha uamuzi wa watu.

**Iwapo ukaguzi utaonyesha kwamba matokeo ya uchaguzi yalikuwa tofauti na yaliyotangazwa na Chebukati, unatarajia Ruto ajiuzulu?**

Kabla ya kufika hapo, kumbuka wakati huu, maandalizi ya uchaguzi yalivyokuwa, kila kitu kilikuwa shwari. Kutoka vituo vya kupigia kura ambapo mpigakura alitambuliwa, upigaji kura, kuhesabiwa, ujumulishaji, kutangazwa katika vituo vya kupigia kura. Kisha kujumlisha na kupeperusha matokeo katika vituo vya ujumulishaji vya maeneo bunge. Kila kitu kilikuwa sawa. Shida hasa ilikuwa kutangazwa kwa matokeo katika Kituo cha Kitaifa cha Ujumlishaji, Bomas of Kenya. Hapo ndipo palikuwa

# Hivi ndivyo tulishida kura, asema kinara wa Azimio

Kutoka Uk 5

wa na maajenti katika vituo vyote 46,000 vya kupigia kura kote nchini. Anadai kuwa katika ngome za mpinzani wake mkuu, Ruto, maajenti wake walidhulumiwa, kupigwa na kuzuiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura.

Kama Raila alikuwa amechoka kutokana na kushindwa katika uchaguzi wa urais na Mahakama ya Upeo kutupa kesi yake, sasa anaonekana akifanya anachokielewa vizuri: kuchochea joto la kisiasa na kufanya walio mamlakani kuacha wanachopaswa kufanya ili kukabiliana naye.

Kando na matakwa kuhusu udanganyifu katika uchaguzi, Raila anaonekana kuridhika kuwa ameikazia serikali ya Ruto iliyoshindwa kusuluhisha matatizo ya kiuchumi na kutimiza ahadi nyingi za kampeni. Pia anazungumzia hadhi ya utawala wa Kenya Kwanza, kuhusu kuondolewa kwa kesi za ufisadi, na uhalifu, zinazowakabili watu wanaopendelewa na kuteuliwa kwao katika afisi za umma.

Anasema wananchi wamegundua kuwa walidanganywa na hivyo wanaelekea kupoteza imani na utawala huu. Anaonekana kulenga kutumia hali hii kuendeleza vita dhidi ya utawala wa Rais Ruto.

Lakini ni lazima Raila ajue pia kuwa huenda anapoteza umaarufu kufuatia hatua ya wanasiasa wa kambi yake kuhamia kwa Ruto. Wanachama wa Azimio katika Bunge na serikali za kaunti wanapungua kwa kasi huku viongozi waliochaguliwa wakishawishiwa kuunga mkono serikali, lakini anaonekana kutotishwa na hali hiyo, akisema mtindo wa wanasiasa kuhamia vyama vingine umekuwepo tangu kurudishwa kwa siasa za vyama vingi.

Ni wazi kuwa, kwa mara nyingine, Raila anajiandaa kwa siasa kali za upinzani. Kwake, mbinu ya kuendeleza siasa hizo ni kuzungumza moja kwa moja na watu badala ya kufanya mikutano ndani ya kumbi.

Anaonya kuhusu kurudi kwa utawala wa kidikteta, siasa za enzi za Nyayo, akisema ndiyo maana Ruto analenga kudhibiti Bunge, kuingilia mahakama, kutisha vyombo vya habari na kubuni IEBC itakayompendelea.

Katika hali hiyo, anasema, hawezi kuwatelekeza wananchi kwa kustaafu siasa. Mnamo Januari 8, mwaka huu aliadhimisha miaka 78 ya kuzaliwa. Wakati wa uchaguzi mkuu wa 2027 atakuwa na miaka 82, lakini anashikilia kuwa bado ana kazi ya kufanya.

Kiongozi wa Wiper Kalonzo Musyoka, mmoja wa washirika wakuu wa Raila, tayari ametangaza azma ya kuwania urais. Lakini Raila anamtaja kuwa kiongozi mtiifu na mkakamavu wa Azimio pamoja na Martha Karua, Wycliffe Oparanya, Hassan Joho na wengine ambao wako tayari kuendesha meli ya Azimio wakati ukiwadia.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

## kurunzi ya kenya

na shida na tulieleza hayo kila wakati. Hatukufurahishwa na kilichokuwa kikifanyika na tulijaribu kumweleza mwenyekiti wa IEBC na timu yake. Tumefanya uchunguzi wetu huru ambao umefichua mifumo iliyokuwa imewekwa na IEBC na washirika wake. Katika kituo cha kupigia kura ambako kulikuwa na kifaa cha kutambua mpigakura cha KIEMS, baada ya kura kujumulishwa na kutangazwa na maafisa wa uchaguzi, walitumia kifaa hicho kupiga picha fomu ya matokeo kisha kuituma kwa sava. Tuligundua kulikuwa na sava nne, moja Uholanzi, moja Venezuela, moja katika jumba la Anniversary Towers na ya nne katika eneo la Viwandani. Katika Bomas, kulikuwa na tovuti iliyopokea na kuonyesha matokeo kutoka kwa sava. Sava iliyo Venezuela ndiyo ilikuwa ikipeperusha matokeo hadi Bomas. Walichokuwa wakifanya ni kupokea matokeo na kuyabadilisha kabla ya kuyawasilisha Bomas.

**Katika kituo cha ujumlishaji, tunaweza kuwa tunazungumzia kuhusu data. Katika kituo cha kupigia kura, nakala halisi za fomu zinazotiwa saini na maajenti wako na pia maajenti wa wagombeaji wengine. Si shida ilikuwa hapo na sio kutoa nakala?**

Hapana, shida haikuwa hapo. Shida ni matokeo yaliyotangazwa...

Kama ungewasilisha Fomu 34A zako zilizothibitishwa, si hiyo ingethibitisha kesi yako kwamba kulikuwa na makosa katika matokeo ya mwisho?

Ni lazima ulinganishe na ukweli wa mambo. Tunachosema ni kwamba kilichokuwa katika tovuti ya umma ni tofauti na kilichokuwa katika sava. Hicho ndicho tunajaribu kuthibitisha, kwamba kilicho katika tovuti ya umma kimebadilishwa, hakionyeshi matokeo halisi yaliyotoka vituo vya kupigia kura.

**Rekodi zenu wenyewe, mlizopata kutoka kwa maajenti wenu katika vituo vya kura, hazingeonyesha tofauti hizo?**

Tuna vituo 46,000 vya kupigia kura. Haiwezekani kuwa na maajenti katika vituo vyote hivyo 46,000 vya kupigia kura.Katika baadhi ya maeneo, maajenti wetu walikuwa wakizuiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura. Katika baadhi ya maeneo, walipigwa na kufukuzwa. Ni vigumu kuwa na maajenti katika vituo vyote vya kupigia kura 46,000. Utakuwa na bahati kuwa nao katika vituo 40,000. Katika maeneo ambayo watu wana chuki na polisi wenyewe wanashirikiana kupinga watu wako, ni vigumu kupata matokeo kutoka vituo vyote 46,000 vya kupigia kura. Bila kuwa nao kila mahali, tofauti unazoonyesha zitapingwa. Hii ndiyo sababu kitu cha muhimu ni kufunguliwa kwa sava. Sava haidanganyi.

**Sasa, wakiruhusu sava ifunguliwe, hawatakuwa wamepata nafasi ya kubadilisha kilicho hapo?**

Hapana. Matokeo yalipigwa picha na kutumwa yalivyo. Kwa hivyo, ukitaka kuthibitisha, nenda kwa sava. Hiyo haiwezi kuvurugwa. Kama mtu atajaribu, utaona kilichofanyika.

**Uchaguzi ulifanywa Agosti 9. Usiku uliofuata, maajenti wako walikuarifu kuwa ulikuwa ukiongoza kwa kura nyingi. Kituo chako cha uchaguzi kilianza kusherehekea, na pengine wakaacha kuwa makini kufuatilia kilichokuwa kikifanyika katika kuhesabu na kujumlisha. Je, ripoti hiyo ya maajenti wako huenda ilikuwa ya mapema? Uliangushwa na timu yako?**

Haikuwa mapema. Ilikuwa wazi maajenti wetu walikuwa wamejua, na hata kura za maoni za baada ya uchaguzi za waangalizi tofauti zilionyesha tulikuwa na zaidi ya asilimia 55 dhidi ya asilimia 42 ya Ruto.

**Turudi kwa swali hili. Ukifaulu kufunguliwa sava na ithibitishwe unasema ukweli, ni kitu gani kitafanyika?**

Swali ambalo linapaswa kujibiwa, na sio kwamba hatuna mantiki kwa sababu tunachozungumzia ni kwa vizazi vya baadaye, ni iwapo kitu hiki hakitachunguzwa vyema na kushughulikiwa hadi mwisho, basi sahau uchaguzi mwingine wa urais katika nchi hii. Nani atahatarisha muda wake akienda kushiriki uchaguzi kama matokeo yanatangazwa kiholela na IEBC inayopendelea? Hii ni IEBC iliyogawanyika. Watatu wanasema haya ndiyo matokeo na wanne wanasema 'la', lakini tunalazimishwa kukubali wachache. Badala yake, wengi waliokataa wanateswa. Hii ni nchi ya aina gani? Sasa wako katika mchakato wa kuunda upya tume peke yao, sasa wanaunda Chebukati saba badala ya watatu. Nani anaweza kuwa mjinga kushiriki uchaguzi unaosimamiwa na tume kama hiyo?

**Ulianza Jumatatu na mkutano wa Kamukunji na ninaamini unapanga shughuli zaidi kama hizo. Ni hatari zipi za mikutano hiyo au malalamishi na maandamano barabarani yanayobadilika na kuwa ghasia?**

Hatutarajii ghasia. Kama kutakuwa na ghasia, zitatoka kwa serikali na watawajibikia athari zake.

Mpango huu umefufua upya nadharia kwamba wewe haukubali kushindwa katika uchaguzi, na kwamba ukishindwa unazua vurugu ili uweze kupata kitu mezani; mfano ni serikali ya nusu mkate ya 2007 na Rais Kibaki kisha handisheki ya baada ya uchaguzi wa 2017 na Rais Kenyatta.

Hiyo ni propaganda duni na ya kipumbavu inayosambazwa na watu wasiowastaarabu. Tumelegeza misimamo kwa maslahi bora ya nchi hii. Kuhusu handisheki yangu na Uhuru, hatukuomba chochote katika serikali. Chama changu hakikuwa na wadhifa hata mmoja katika serikali, hata hakuna aliyeteuliwa waziri msaidizi. Hatukuwa katika serikali. Watu wanaopiga kelele ndio walikuwa ndani ya serikali. Chochote tulichoomba kilikuwa katika BBI. Ukiangalia MOU tuliyotia saini na Uhuru, tulikubaliana tungefanya mabadiliko ili chaguzi zijazo ziwe huru na za haki. Na uchaguzi ulikuwa huru na wa haki hadi mchakato wa mwisho wa ujumlishaji katika Bomas of Kenya.

**Tunachoona katika ushahidi mpya ni takwimu tu. Mmefanya nini kuchunguza takwimu hizo na kuridhika kwamba mlichopatiwa ni kweli na halali?**

Kufikia sasa, IEBC ingekuwa imejitokeza na kupinga takwimu hizo. Wanaweza tu kuzipinga kwa kutoa zile sahihi. Nakala za Fomu 34B zilizotolewa na mfichuzi, fomu za matokeo kutoka vituo vya ujumlishaji vya maeneobunge, zina muhuri wa IEBC, saini ya Afisa wa Uchaguzi, zimetiwa saini na maajenti wa vyama, Azimio na UDA. Muhimu zaidi, zina nambari ya kipekee inayoweza kukupatia habari kuhusu mahali na wakati ilipigwa picha na kupeperushwa, eneo, tarehe na wakati. Huwezi kughushi hayo. Kama IEBC ina fomu mbadala, inaweza kuzitoa.

Kulikuwa na maeneo bunge 245 wakati huo. Hii ilikuwa Agosti 10. Watu walipiga kura Agosti 9. Na matokeo ya maeneo bunge hayo 245 yalikuwa tayari Agosti 10. Wameeleza kwamba 45 yaliyobaki yalipelekwa moja kwa moja Bomas na maafisa wa uchaguzi ambapo picha zilipigwa na kupakiwa katika tovuti ya IEBC na kuongezwa. Ukijumuisha, Ruto anapata kura 5.9 milioni na tunapata kura 8.1 milioni. Ni za kweli, haziwezi kupingwa. Hizi zinatoka kwa mfanyakazi wa ndani wa IEBC aliyezipata kutoka kwa Sava katika Anniversary Towers.

**Kuhama. Ni juzi tu ambapo wabunge wa Azimio wa chama cha Jubilee walikutana na Ruto. Karibu kutoka siku ya kwanza, makundi tofauti ya Wabunge yamekuwa yakihamia upande wa Ruto. Hatua hii inakudhoofisha na kwa kiwango gani na kuathiri mpango wako wa kisiasa?**

Kuhama sio kitu kigeni hapa. Kumbuka kurudishwa kwa siasa za vyama vingi, Bunge la saba, ndani ya siku chache, chama cha Kanu cha Rais Moi kilikuwa kikinunua wabunge wa upinzani. Kulikuwa na Apili Wawire wa Lugari, Protus Momanyi wa Bonchari, Owini Likowa wa Migori, na wengine wengi. Kitu muhimu ni kwamba watu wanaohama katika kiwango cha kitaifa, katika Bunge, hawana athari zozote mashinani, kilicho muhimu ni watu.

**Hivi majuzi, Ruto alikaribishwa na viongozi wa Azimio waliochaguliwa Nyanza ambao walikubali kushirikiana naye katika maendeleo. Sasa unasema Azimio haimtambui Ruto kama rais halali. Huu sio mkinzano?**

Hapana, hakuna mkinzano hapa. Watu hawamtambui yeye kama mtu binafsi, wanatambua taasisi. Kumbuka tulikuwa na warsha na magavana, na wakasema Katiba inasema serikali ya kitaifa na za kaunti ni tofauti, lakini lazima zishirikiane. Kuna majukumu ambayo ni ya serikali ya kitaifa na ambayo ni ya serikali za kaunti. Kutambua hilo hakumaanishi kutambua jinsi mtu alipata urais.

**Ulipoingia katika handisheki na Uhuru, ulianza kutetea serikali. Ulionekana kuacha msimamo wako kama mtetezi wa waliotengwa, wanyonge na wanaoteswa. Ruto alichukua jukwaa lako na Vuguvugu la Hasla. Hilo halikukuweka katika hatari?**

Hiyo ni propaganda ya wanahabari. Sikubadilisha msimamo. Makubaliano yetu yalikuwa kwamba tungefanya mageuzi, lakini Uhuru angeendelea kuendesha serikali na timu yake iliyojumuisha Ruto. Lakini Ruto hakutaka mkataba niliotia saini na Uhuru, MOU, kwa sababu alikuwa akihusika na mipango yake ya urithi. Kila wakati mambo yalipokuwa yakiharibika, nilikuwa nikimwambia Uhuru. Kuna wakati nilikuwa nikitangaza wazi. Sijawahi kuacha jukumu langu. Nilishauri wabunge waendelee kutekeleza jukumu lao la kikatiba la kukosoa serikali. Bila

Endelea Uk 8

kurunzi ya kenya

Kutoka Uk 7

shaka Ruto alikuwa akiendesha siasa za kujitafutia umaarufu, akikosoa serikali ambayo alikuwa akuhudumia.

**Azimio ilikuwa chombo spesheli cha uchaguzi. Itadumu kuelekea 2027?**

Imeungana kwa wakati huu. Miungano hudumu kutimiza kusudi fulani. Inaweza kukua kuwa vuguvugu rasmi, au inaweza kusambaratika, kwa kutegemea hali. Kuna nia njema kwa sasa na imeamua kuendelea kushirikiana licha ya juhudi za serikali ya Kenya Kwanza kuhujumu umoja wake kwa kununua wabunge kwa pesa kidogo.

**Na maisha yako binafsi ya kisiasa kuelekea 2027, na umri wako, una mpango wa mrithi katika siasa za ODM na Nyanza katika hali ambayo viongozi ibuka hawana mvuto?**

Kwanza, elewa kwamba siasa zangu sio za Nyanza, lakini ni za Nairobi na kitaifa, sio suala la umri. Nina nguvu sana na ninaweza kuendelea, lakini niko tayari kuachia wengine wakati utakapofika. Nina watu ninaoshirikiana nao ambao wamekuwa waaminifu na imara kama Kalonzo Musyoka. Tuna Martha Karua ambaye ni imara na mwenye msimamo,Wycliffe Oparanya, Hassan Joho, Jeremiah Kioni na wanasiasa wengi vijana ambao wana uwezo wa kuongoza Azimio.

Hatujapungukiwa na watu wa kuturithi. Siko tayari kustaafu kwa kuwa watu hawajasema, na siwezi kuacha siasa wakati hali inaonekana kuwa mbaya. Hata kama wanasema tusahau ya 2022, itakuwaje kwa nchi? 2027 itakuwa tofauti kweli wakati walio mamlakani sasa wanapanga njama ya kuunda tume ya uchaguzi watakayodhibiti na tayari wanatisha wanahabari na kushinikiza kufutwa kwa wanawaona kuwa wapinzani wa ajenda zao? Tutakuwa na vyombo vya habari vinavyowatumikia na idara za serikali wanazodhibiti, tunaelekea kurudi katika mbinu za Nyayo. Hali ya baadaye ni mbaya, kwa hivyo huu sio wakati wa kuzungumzia kustaafu.


*- Imetafsiriwa Na Benson Matheka*

■ JOTO LA UCHAGUZI LISILOSHUKA

# LAANA YA KAMPENI

## Kupanuliwa kwa demokrasia kumetumbukiza nchi katika hali ya kampeni za uchaguzi zisizokuwa na kikomo

● Na OSCAR OBONYO




Jumatatu iliyopita, Rais William Ruto alifika katika mazishi ya dada ya Waziri wa Biashara Moses Kuria katika kijiji cha Wamwangi, eneo bunge la Gatundu Kusini akiandamana na naibu wake, Rigathi Gachagua. Waliofuatilia kwa makini staili ya kuwasili kwao na ujumbe wa hotuba zao za kisiasa, waligundua zilikuwa sawa na kampeni zao za uchaguzi miezi mitano iliyopita.

Kufuatia kuchaguliwa kwao kama Rais na Naibu Rais mnamo Agosti 9 na kuapishwa kwao kuingia mamlakani Septemba 13, itifaki inahitaji kwamba Gachagua angewasili mapema katika eneo la mazishi ili amkaribishe rasmi mkubwa wake.

Lakini mara nyingi haijakuwa hivyo. Sio tu kwamba huwa wanafika katika hafla wakiwa pamoja, lakini jinsi tu walivyokuwa wakifanya wakati wa kampeni, wawili hao wanaendelea kupuliza parapanda ya kampeni na kuchemsha ngome zao miaka mitano kabla ya uchaguzi mkuu ujao.

Katika mazishi ya Pauline Nyokabi Kuria, kwa mfano, jina la kiongozi wa upinza Raila Odinga lilitajwa sana katika hafla hiyo iliyopaswa kuwa ya maombolezi, huku Rais akionya mpinzani wake mkuu katika uchaguzi mkuu uliopita kuhusu makabiliano ambayo hakufafanua na naibu wake akikemea wanamuziki waliotunga na kuimba nyimbo za kampeni kumuunga mkono Odinga. Waliozungumza katika hafla hiyo walikuwa wakijibu hotuba katika uwanja wa Kamukunji ambapo Raila aliongoza vigogo wa Azimio La Umoja Martha Karua na Kalonzo Musyoka kushambulia kwa maneno serikali ya Kenya Kwanza.

Odinga alisema kwamba muungano wake hautamtambua Ruto kama Rais wa tano wa Kenya wakidai kura zao ziliibwa.

Shughuli za Jumatatu, ingawa zinahusu madai ya wizi wa kura katika uchaguzi, zinaonyesha desturi ibuka ya kisiasa Kenya ya kampeni zisizokoma za uchaguzi ambazo huanza punde tu kila baada ya uchaguzi na kuendelea kwa miaka. Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Demokrasia ya Vyama Vingi, Franklin Mukhwanja, anahusisha mtindo huu na ukosefu wa mfumo katika Katiba ya 2010 ambayo muundo wake wa utawala unaacha nje wanaoshindwa katika uchaguzi wasiweze kushikilia viti vya kisiasa, ikiwemo katika Seneti na Bunge la Kitaifa

Hii, anasema Mukhwanja, inaacha wanaoshindwa uchaguzini - hasa uchaguzi wa urais unaokuwa na ushindani mkali - bila jukwaa la kisheria au njia ya kuungana na wafuasi wao. "Ni vipi, kwa mfano, unatarajia Raila kudumisha matumaini ya wapiga kura zaidi ya 6.8 milioni waliounga mkono azma yake bila kuwa na jukwaa rasmi isipokuwa katika mikutano ya kisiasa, ambayo wakati mwingine inaweza kukumbwa na ghasia?"

Wataalamu wa masuala ya Uchaguzi wanakubaliana kuwa tatizo linazidishwa na aina ya uchaguzi wenye ushindani mkubwa, ambao nchini Kenya unaendeshwa na sera ya mshindi kutawala kila kitu. Na, kulingana na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa iliyokuwa Tume ya Uchaguzi ya Kenya, Gabriel Mukele, "upofu wa kuagiza demokrasia kutoka Amerika" unafaa kunalaumiwa kwa baadhi ya athari mbaya.

Katika utafiti wao, Gharama ya Siasa Kenya: Athari za Ushiriki wa Siasa na Maendeleo, Profesa Karuti Kanyinga na Tom Mboya wanataja kuongezeka kwa ushindani wa kisiasa katika viwango vyote tangu 2013, kufuatia Katiba ya 2010. Wanasema mfumo wa uchaguzi wa mshindi kutwaa mamlaka yote unatenga kabisa wanaoshindwa, "na hivyo basi kusababisha hali ya kufa au kupona katika ushindani wa kisiasa".

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya kenya

PESA ZA NOTI



De La Rue haitarajii kupata maagizo mapya kutoka kwa Benki Kuu ya Kenya katika kipindi cha miezi 12 ijayo. PICHA | MAKTABA

# KISIMA CHA KUCHOTA PESA SASA CHAKAUKA

## Kandarasi kubwa na ya miaka mingi ya kuchapisha pesa kati ya kampuni ya Uingereza ya De La Rue na Serikali ya Kenya inaonekana kuelekea kufikia mwisho

• Na JAINDI KISERO

Tangazo la kampuni ya kuchapisha pesa ya Uingereza, De La Rue, kuwa haitarajii kupata maagizo mapya kutoka Benki Kuu ya Kenya kwa miezi 12 ijayo, pengine ni ishara kuwa serikali mpya ya Rais William Ruto inafikiria kupatia kampuni mpya ya kuchapisha pesa kandarasi hiyo.

Ni hatua muhimu kwa kuwa Kenya haijawahi kutangaza tenda ya kimataifa yenye ushindani ya pesa za noti tangu Benki Kuu ya Kenya ilipoanziahwa 1966.

Kandarasi hiyo imekuwa ikipewa tu kampuni ya De La Rue isipokuwa kati ya 1966 na 1985, wakati noti za benki za Kenya zilichapishwa na kampuni ya Uingereza iliyofahamika kama Bradbury & Wilkinson ambayo baadaye ilinunuliwa na De La Rue.

Kampuni hiyo ya Uingereza iliyoungwa mkono sana na wanasiasa Kenya wakati wa utawala wa aliyekuwa Rais Daniel arap Moi, ilijenga kiwanda cha kuchapisha pesa za noti jijini Nairobi, kiwanda cha pekee cha aina hiyo Afrika. Kiwanda hicho kilichoko katika eneo la Ruaraka kilijengwa 1992.

Wiki iliyopita, De La Rue pia ilitangaza kuwa imesimamisha uchapishaji nchini Kenya na ikafuta wafanyakazi zaidi ya 300.

Ni majuzi tu kampuni hiyo ilipoagizwa na Mahakama Kuu ya kulipa Mamlaka ya Ushuru Sh1.1 bilioni baada ya kushindwa katika kesi iliyochukua miaka mingi.

Ingawa habari za wafanyakazi zaidi ya 300 kufutwa kazi ndizo ziligonga vichwa vya habari, ni wazi kuwa matukio ya wiki iliyopita yataibua mjadala kuhusu iwapo serikali ilichukua hatua iliyofaa kununua asilimia 40 ya hisa katika tawi la humu nchini la De La Rue na iwapo mlipa ushuru alifaidika kutokana na ununuzi huo.

Mkataba wa ushirika kati ya serikali na De La Rue ulitiwa saini Agosti 2018 lakini haukukamilishwa hadi Aprili 2019. Tangu wakati huo, De La Rue Kenya haijawahi kupata faida au kutangaza mgao kwa serikali kwa madai kuwa serikali haijaipatia nafasi ya kushindana katika miradi ya humu nchini kama vile uchapishaji wa stampu za ushuru, stampu za Shirika la Ubora wa Bidhaa Kenya, na za uidhinishaji za Shirika la kukabiliana na bidhaa feki.

Ushahidi mpya ambao Darubini ya Wiki imeona unaonyesha huu ulikuwa mkataba wa pamoja uliofaidi upande mmoja ambao ulipatia kampuni hiyo manufaa mengi kuliko serikali.

Mnamo Februari 2015, serikali ilipatia kampuni ya uwekezaji ya Benki ya Commercial Bank of Africa kazi ya kukagua vitabu vya hesabu vya tawi la kampuni ya De La Rue International eneo la Ruaraka. Katika stakabadhi inayoitwa Mradi Kifaru, benki hiyo ya uwekezaji ilitoa maelezo ambayo yangeonya serikali kuhusu kilichoendelea katika ushirika huo.

Benki hiyo iligundua kuwa hata baada ya serikali kuuziwa asilimia 40 ya hisa, De La Rue ilikuwa na muundo uliofanya shughuli zake Kenya kuwa tawi tu la makao yake makuu - kwamba ilikuwa mateka wa kupewa maagizo kuhusu maamuzi muhimu, ikiwemo uuzaji na ununuzi.

Kampuni ya CBA Capital iligundua kuwa shughuli za De La Rue Kenya zilikuwa tu moja la maeneo sita ya utengenezaji ya kampuni hiyo ya uchapishaji ya Uingereza, maeneo mengine yakiwa Amerika, Uingereza, Malta, China na Sri Lanka. Washauri hao waligundua kuwa wauzaji wakuu wa vifaa muhimu katika maeneo ya utengenezaji kama vile karatasi, pleti na wino walihusishwa na kampuni za kundi hilo.

Kutokana na hilo, washauri hao waligundua kuwa, kiwango cha uuzaji kati ya kundi hilo kilikuwa kikubwa. Kwa mfano, mnamo 2010, asilimia 88 ya mauzo ya De La Rue Kenya yalienda kwa kampuni mshirika mkuu London.

Ununuzi ndani ya kundi hilo pia uligunduliwa kuwa wa kiwango cha juu cha asilimia 61 mnamo 2011. Hivyo basi, kinachotajwa katika ripoti hiyo ni operesheni iliyo na mianya mikubwa ya kulipa ushuru wa chini, kuhamisha faida na hata kutorosha pesa.

Ripoti ya CBA pia iligundua kuwa MNC pia ilikuwa ikitoa faida kubwa kutoka tawi la humu nchini kupitia ada za usimamizi.

Haikuwa ajabu basi, kwamba baada ya kuanza kazi ya uchapishaji, shughuli za pamoja zilizua mzozo mkubwa na shirika la ukusanyaji ushuru. Kwanza, kampuni hiyo imekuwa na kesi ya miaka mingi ya ushuru wa VAT wa Sh1.2 bilioni ambayo iliamuliwa na Mahakama Kuu majuzi.

Pili, mzozo wa miaka mingi wa ushuru wa kampuni wa 2013-2017 ulizuka baada ya KRA kufanyia De La Rue ukaguzi wa kuhamisha faida ilipogunduliwa kuilikuwa ikilipa mrabaha mkubwa kampuni mshirika wake mkuu ya Uingereza.

Zaidi ya haya yote ni kesi nyingine ambayo kwa sasa inashughulikiwa na mfumo mbadala wa kutatua mizozo inayohusu ulipaji wa mirabaha 2018 na 2019.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

■ NI HALI YA PATA POTEA KATIKA JUBILEE

# MISIMAMO YABADILIKA

## Ruto anaendelea kupenya ngome ya Jubilee huku wanasiasa walioshindwa kwenye uchaguzi mkuu katika eneo la Mlima Kenya na kote nchini wakielekea chama tawala

● NA OSCAR OBONYO

Alikuwa sura ya ukaidi na matumaini katika kambi ya Raila Amolo Odinga wimbi la kisiasa la William Samoei Ruto lilipofagia eneo la Mlima Kenya kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana. Lakini miezi minne baada ya Dkt Ruto kuapishwa kuwa Rais, Mbunge Mteule Sabina Chege analaumiwa kwa kuongoza katika kujiunga na upande wa serikali hatua ambayo inaweza kuwa mwanzo wa mwisho wa chama cha Jubilee.

Katika wiki moja iliyopita, Chege, pamoja na baadhi ya wabunge waliochaguliwa kutoka Jubilee, wamefanya mikutano, kwanza na Naibu Rais Rigathi Gachagua na Jumatatu iliyopita na Rais, siku ambayo muungano wa Azimio La Umoja ulifanya mkutano wa hadhara katika uwanja wa Kamukunji, Nairobi na kutangaza serikali ya Ruto kuwa "haramu".

Siku na wakati wa mkutano huo wa kiamsha kinywa katika Ikulu unaibua maswali na inaeleweka ni kwa nini kuwepo kwa Chege katika hafla hiyo ni muhimu kwa muungano unaotawala wa Kenya Kwanza na pigo kwa Azimio.

Chege ni mwanasiasa wa hadhi ya juu katika muungano wa Azimio, ambapo ni mwanachama Baraza la Muungano, ambalo mwenyekiti wake ni aliytekuwa Rais Uhuru Kenyatta. Kwa hivyo, juhudi za Ruto kumnyakua Chege, ambaye pia ni Naibu Kinja wa Wachache katika Bunge la Kitaifa, ni mkakati wa kisiasa.

Chege, ambaye alikuwa Mbunge wa Kaunti ya Murang'a kwa mihula miwili ni mmoja tu wa vigogo wengi wa kisiasa kutoka eneo la Mlima Kenya ambao Kiongozi wa Wengi katika Bunge la Kitaifa Kimani Ichung'wa anatabiri kwa furaha kuwa watavuka "upande wetu" hivi karibuni. Mwanachama mwingine mkuu wa Azimio, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki Kanini Kega, ambaye ni mkurugenzi wa chaguzi wa Jubilee, pia amehudhuria mikutano iliyoandaliwa na viongozi wa Kenya Kwanza.

Chege anakanusha kuhusika kwa vyovyote katika mpango wa kudhoofisha chama cha Jubilee, akishikilia kuwa yuko ndani ya kilichokuwa chama tawala na mwaminifu kwa Kenyatta, ambaye kila mara humtaja kuwa "kiongozi wa chama changu". Amekerwa na ripoti zinazomhusisha na chama cha Ruto cha United Democratic Alliance (UDA). "Kwa nini linakuwa suala la mjadala wa kitaifa watu wa jamii yangu ya Wakikuyu wakishauriana na Rais kuhusu masuala ya maendeleo yao, ilhali watu wa jamii zingine, wakiwemo Wakisii, jamii za kaskazini mwa Kenya na Waluhya pia wameshauriana naye Ikulu bila kulaumiwa?"



Mbunge Mteule Sabina Chege alikutana na Naibu Rais Rigathi Gachagua. PICHA | MAKTABA

Wakati huo huo, Rais na washirika wake wa kisiasa wanaendelea kupenya katika eneo la Jubilee.

Nguzo nyingine muhimu katika kampeni ya Azimio, Priscilla Nyokabi, ambaye aligombea kiti cha Useneta Nyeri, anaripotiwa kukaribia kuhama. Wiki mbili zilizopita, mbunge huyo wa zamani wa Kaunti ya Nyeri aliandamana na Rais hadi Kisumu katika ziara yake ya hivi majuzi eneo la Nyanza.

Wanasiasa wengi eneo la Mlima Kenya - na kote nchini – ambao walishindwa katika uchaguzi uliopita, wanahamia kimya kimya katika chama tawala. Huu ni mtindo wa kawaida katika siasa za Kenya na ambao humpa kiongozi aliye mamlakani faida kubwa dhidi ya wapinzani wake wa kisiasa.

Akizingatia ukweli huu, Katibu Mkuu wa chama cha Jubilee, Jeremiah Kioni, anaapa hata hivyo kusonga mbele bila kujali "maamuzi ya watu fulani kubadilisha misimamo yao katikati". Mbunge huyo wa zamani wa Ndaragwa anashikilia kuwa ni bora kuandamana na watu wachache waliojitolea kuliko umati wa watu, "baadhi yao kwa kujua au kutojua kuwa wanazuia harakati za haraka kuelekea lengo lililowekwa".

Afisa huyo wa Jubilee ameanzisha kampeni kali ya takwimu, ambayo inaonekana kuwasumbua sana washirika wa Ruto. Akitumia ufichuzi wa afisa asiyejulikana wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Kioni anadai kuwa Odinga alishinda uchaguzi wa Agosti na anashikilia kuwa watu wa Mlima Kenya "wanataka kuhakikisha kuwa kura zilizopigwa kumuunga mkono Raila ni muhimu na ni haki yetu kikatiba kudai hilo". Ichung'wa kwa upande wake anasema kushindwa kwa Jubilee kulisababishwa na "uongozi wa Uhuru Kenyatta", hatua ambayo imeweka chama hicho "katika mkondo sawa na vyama vingine tawala vya zamani".

Akidai kuwa hakuna mtu yeyote – wakiwemo waliochaguliwa kwa tikiti ya chama hicho – anayetambua Jubilee chama chaguo lake, Mbunge huyo wa Kikuyu anatabiri kuwa "watu wote hatimaye wahama chama hicho na pengine kumuacha Jeremiah Kioni pekee".

Kwa upande wake, aliyekuwa Mbunge wa Nyeri Mjini Ngunjiri Wambugu anaamini Jubilee imejipata katika changamoto hizo "kwa sababu ya ukosefu wa uongozi". Isipokuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, ambaye ameibuka

Nation Media Group "Digital Copy"

## kurunzi ya kenya

kuwa sura ya chama kwenye hafla za umma, maafisa wote wa chama, akiwemo kiongozi wake Uhuru Kenyatta, wanaonekana kutoweka. Wambugu anasema Kioni haionekani kuwakilisha cheo wala sura yoyote ya chama. Baadhi ya washirika wa Uhuru Kenyatta wanasema Rais huyo wa zamani hawezi kumkabili kisiasa mrithi wake. Hata hivyo, Kenyatta amekuwa akiendesha mambo kwa mbali kutokana na matamshi na vitendo vya washirika wake.


Kwa mfano, awali, Kioni alionekana kumshambulia mgombea urais wa Azimio na hata kupendekeza Oktoba mwaka jana kuwa Jubilee na watu wa Mlima Kenya walikuwa wamemlipa Odinga deni la kisiasa alilowadai wakati wa kupiga kura na walikuwa tayari kuvunja uhusiano naye.

Aliongeza: "Mambo yakiharibika jamii hukimbia na kukusanyika pamoja. Kinachoonekana kutawala ni uaminifu kwa jamii na dalili ziko wazi. Si hoja kama uko UDA au Kenya Kwanza." Lakini alibadilisha msimamo huobaada ya kile wadadisi waliamini kuwa ngizo kutoka kwa kiongozi wa chama chake.

Akisisitiza kuwa Jubilee inawakilishwa katika Bunge la Kitaifa na katika mabunge ya kaunti kote nchini, Wambugu anasema chama cha Jubilee kinapokea ufadhili wa umma kutoka kwa serikali, kwa hivyo kiko hai na kinaweza kuwa thabiti tena: "Lakini kinahitaji tathmini kamili ya kile kinachosimamia leo. Tunahitaji kutathmini ni kwa nini tulishindwa vibaya sana katika chaguzi zilizopita na kupata viongozi wapya wanaoweza kufanya kazi katika uhalisia wa kipindi hiki cha siasa za sasa kwa nia ya kurudisha chama hiki kwenye mkondo mkuu wa siasa za kitaifa".

Pia kuna vita vya ubabe eneo la Mlima Kenya ambavyo Jubilee inaweza kutumia kujijenga. Kuibuka kwa Naibu Rais Rigathi Gachagua kuwa msemaji wa Mlima Kenya hakujakubaliwa na watu wote. Kisha kuna Waziri wa Biashara Moses Kuria, ambaye anataka kujionyesha kama kigogo wa kisiasa wa eneo hilo.

Suala hili tayari limezua ugomvi kama ilivyoshuhudiwa Jumatatu iliyopita wakati wa mazishi ya dada ya Kuria eneobunge la Gatundu Kusini. Akizungumza katika hafla hiyo, mfanyabiashara mashuhuri na mshirika mkuu wa Rais, Mary Wambui, alimlaumu vikali Mbunge wa eneo hilo Gabriel Gathuka Kagombe kwa madai ya kumdharau Kuria. Wambui, aliyeteuliwa majuzi Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Kenya anamchukulia Waziri huyo kuwa "tegemeo la watu wetu siku z usoni".



Naibu Rais Rigathi Gachagua akiwa na Mbunge Mteule Sabina Chege. Gachagua alikutana na kundi la Wabunge wa Jubilee katika jumba la Harambee House Annex Januari 20. PICHA I DPCS



Katibu Mkuu wa Jubilee Jeremiah Kioni akihutubia wanahabari katika afisi za Jaramogi Oginga Odinga Foundation mnamo Januari 18. PICHA I LUCY WANJIRU

Jambo la kushangaza ni kuwa Gavana wa Kiambu Kimani Wamatangi hakuhudhuria hafla hiyo, ambayo wadadisi wanaihusisha na tofauti za kisiasa. Kisha kuna magavana wa zamani Mwangi wa Iria (Murang'a) na William Kabogo (Kiambu), ambao pia wamo kwenye vita vya kisiasa katika eneo hilo.

Kwa sababu Jubilee ndicho chama kikubwa zaidi katika eneo la Mlima Kenya ambacho uongozi wake mkuu ni wa mashinani, mizozo ya kisiasa na kung'ang'ania mamlaka katika eneo hilop inaweza tu kuwa na manufaa kwake. Jubilee, Wambugu anashauri, lazima kijitahidi kubakia hai, la sivyo kitafuata njia ya vyama tawala vilivyotangulia.

Kwa mfano, tangu kiliposhindwa vibaya na Muungano wa National Rainbow Coalition (Narc) 2002, chama cha Kanu hakijawahi kupata nafuu kisiasa. Nguvu zake katika Bunge na ushawishi kote nchini zimekuwa zikipungua kila mwaka wa uchaguzi kiasi kwamba kiongozi wake, Gideon Moi, alishindwa kutwaa tena kiti chake cha useneta katika Kaunti ya Baringo.

Chama cha Narc kilikuwepo kwa muda mfupi zaidi wa miaka mitano tu, kutokana na mivutanop ya ndani iliyotokana na makubaliano ambayo hayakutimizwa kuhusu ugawanaji wa mamlaka. Baada ya kuwa mamlakani kwa miaka miwili pekee, Kibaki, upande mmoja, na upande mwingine wanasiasa walioungana na Raila Odinga na Kalonzo Musyoka katika Chama cha Liberal Democratic, wakichukua mielekeo tofauti.

Mzozo huo ulimaliuzima vibaya katika uchaguzi wa 2007, Odinga akiwa mgombea urais wa Orange Democratic Movement (ODM) naye Kibaki akigombea kwa tiketi ya Party of National Unity (PNU), ambacho iliundwa kwa haraka Septemba 2007 baada ya mshirika wa Odinga, Charity Ngilu (ambaye alikuwa amesajili Narc) kukataa kusalimisha chama kwa Kibaki kwa nia yake kuchaguliwa tena. PNU kilianza kama muungano wa vyama kadhaa, vikiwemo Kanu, Narc-Kenya, Ford-Kenya, Ford-People, Democratic Party, Shirikisho na National Alliance Party of Kenya.

Leo hii, Narc, chake Ngilu hakina nguvu tena, chama kilichonguruma kama simba na kung'oa mamlakani cha tangu uhuru cha Jomo Kenyatta, Tom Mboya na mashujaa wengine. Chama kingine kinachopigania uhai wake kisiasa ni PNU, ambacho uongozi wake ulibadilika kutoka kwa Kibaki hadi Makamu wa Rais wa zamani Profesa George Saitoti na sasa kinaongozwa na aliyekuwa Waziri wa Kilimo Peter Munya.

Chama cha TNA cha Kenyatta, alichotumia kugombea urais 2013, kilipoteza umaarufu wake kisiasa alipokiacha chini ya mpango wa muungano na chama cha Ruto cha United Republican Party (URP) na vyama vingine kama Kanu na PNU kuunda Jubilee alichotumia kuchaguliwa tena 2017.

***oscar.tko@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

# habari kwa picha



Aliyekuwa mpiganaji ngumi na mateke raia wa Uingereza na pia Amerika Andrew Tate azungumza na wanahabari akiondoka katika kituo cha kupambana na uhalifu wa kupangwa na ugaidi nchini Romania baada ya uchunguzi wa kidijitali wa vifaa ambapo alihitajika mjini Bucharest, Romania mnamo Januari 25. PICHA | AFP



Waumini wa madhehebu ya Orthodox nchini Ethiopia wakishiriki maombi wakati wa sherehe za Epiphania kwenye ufuo wa Ziwa Batu mnamo Januari 19. PICHA | AFP



Mwanamitindo akionyesha mavazi ya kampuni ya Viktor & Rolf wakati wa msimu wa 2023 wa Wiki ya Mitindo ya Mavazi jijini Paris, Ufaransa, Januari 25. PICHA | AFP



Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron (kushoto) akisalimiana na Rais William Ruto, kabla ya mkutano katika Ikulu ya Rais ya Elysee jijini Paris mnamo Januari 24. PICHA | AFP




Polisi wa kupambana na fujo wakamata muandamanaji mapigano yalipozuka miongoni mwa watu waliokuwa wakiandamana dhidi ya serikali ya Dina Boluarte jijini Lima, Peru, mnamo Januari 24. PICHA | AFP



Wazimamoto wajaribu kuzima moto katika kijiji cha Guryong, mmoja wa mitaa ya mabanda iliyobaki Korea Kusini, eneo la kusini mwa jiji la Seoul Januari 20. PICHA | AFP



Wapiganaji wa Amabutho Zulu wamchoma mkuki askari wa Uingereza aliyeanguka chini wakati wa kuigiza Vita vya Isandlwana, eneo la Isandlwana, Afrika Kusini, mnamo Januari 21. Uigizaji huo hufanywa kila mwaka. PICHA | AFP

Nation Media Group "Digital Copy"

Jukwaa La
Vijana



# MAISHA TIMAMU

*Kevin Mwangi amejitolea katika miaka 20 iliyopita kuhamasisha wateja wake kuishi maisha timamu*


NAFASI YA VIJANA

# Uimarishaji vijana unafaa kuanza kwa mafunzo

**Ujenzi wa taifa:** Ni lazima kila shirika lijiulize iwapo limechangia chochote katika kuunda kikosi thabiti cha wafanyakazi

● NA MOSES OJUANG'

Nchi inayowekeza kwa vijana wake; inayowapa vijana wake mafunzo ya kutosha kwa maendeleo ya siku za usoni ni nchi iliyo katika mwelekeo unaofaa. Ni nchi inayofahamu vyema wajibu. Ni nchi yenye ufanisi. Vivyo hivyo, serikali ambayo sera zake hazigusii chochote kuhusu vijana, ambayo mtazamo wake kuwahusu umegubikwa na masuala mengine inayochukulia kuwa muhimu zaidi ni serikali bure. Ni ukosefu wa uwezo wa kuongoza; ni raia wanaoishi kiholela kuelekea maangamizo ya hakika.



Tunajipiga kifua kuwa na miradi mingi ya kuinua vijana katika nchi yetu na kupongeza juhudi zote zinazoelekezwa kwa suala hilo.

Nyakati zinabadilika kwa kasi na tunahofia hatujitahidi vya kutosha jinsi ilivyo. Tunaona kuwa mambo rahisi sana tuliyokuwa tukifanya hapo zamani yamepitwa na wakati; nyoyo zimekolea uozo katika ubinafsi na kutojali maslahi ya wengine hadi tunapoteza mwelekeo. Miongo michache iliyopita, kozi za vituo vya mafunzo zilikuwa zinakamilika tu baada ya mwanafunzi kupata mafunzo ya kazi anayosomea.

Hapa ndipo nadharia zote na ujuzi zilikuwa zinatiwa makali na mtu mzima aliyeundwa akaundika kuibuka kama mweledi katika jamii.

Lilikuwa sharti rahisi na kwa namna fulani nafasi ya kufanya hivyo ilikuwepo ambapo kampuni, mashirika, viwanda na wafanyakazi wengine walikuwa daima wanasubiri kwa hamu kufika kwa vijana hao waliokuwa tayari kufanya kazi na kujifunza.

Kwa kweli, baadhi ya mashirika haya yalikuwa yenye ukarimu sana kwa vijana hawa na yangechukua hatua zaidi kuwapokea, kugharamia usafiri wao kutoka nyumbani hadi kazini na kurudi na hata kuwalipa kiasi kidogo cha pesa za kukidhi mahitaji yao kwa kipindi cha miezi mitatu walichokuwa hapo.

Mengine hayakuwa na ukarimu kiasi hicho labda kutokana na ukosefu wa sera kuhusu jinsi ya kutunza wafanyakazi hao wanafunzi au kutokana na ubinafsi wa mabosi wake.

Hata wafanyakazi wa muda mrefu mara kwa mara wangewapeleka wanaume na wanawake hao wachanga kwa chakula cha mchana au hata burudani nyakati za jioni siku za Ijumaa.

Mfumo huu ndio uliozaa mameneja wote wazuri tunaojivunia siku hizi. Hatukuwahi kamwe kufikiri kuwa mambo yangebadilika haraka namna hiyo na kuzorota kabisa.

Siku hizi, ni kawaida kukutana na vijana wa kiume na wa kike wakiingia karibu kila kampuni kutafuta nafasi ya mafunzo ya kikazi; ni lazima unamjua mwanamke mchanga anayezunguka mashirika yote mchana kutwa akitafuta nafasi ya mafunzo ya kikazi; mwanamume mchanga aliyechoka na kukata tamaa akiwa ameketi kwenye bustani baada ya wiki nzima ya kuvunjwa moyo; dada ya rafiki ambaye binamu wa shangaziye anatafuta nafasi ya kupata mafunzo. Ni hali ngumu.

Baadhi ya watu waovu hata wanadai hongo ili "kusaidia" kupata nafasi ya mafunzo ya kikazi wanaotafuta nafasi hizo adimu! Wamesahau kabisa kuwa wao wenyewe walisaidiwa. Ni lazima mambo yabadilike katika nchi hii.

Ni lazima vijana wapewe motisha na kila shirika ni lazima lijiulize iwapo limechangia chochote katika kuunda kikosi thabiti cha wafanyakazi. Ikibidi, ni lazima mashirika yote yalazimishwe na serikali kutekeleza jukumu lake la kijamii.

*Bw Ojuang' huchangia kuhusu masuala ya kijamii. mojuang@gmail.com*

*Je, una maoni yoyote kuhusu masuala ibuka? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni yako kwa: weeklyreview@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

## WANAVYOSEMA



**Michael Asule**

Matokeo ya hivi majuzi ni ishara ya bidii na kujitolea kwa walimu pamoja na wanafunzi. Inatia moyo kuona kuwa matokeo yameimarika kutoka mwaka uliopita, huku kiwango cha jumla cha alama za kupasi kikiongezeka. Ni lazima tuendelee kujitahidi kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha kila mwanafunzi anapata nafasi ya elimu bora. Huu ndio mwelekeo,

*- Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta*



**Oscar Mumaraki**

Baadhi ya maeneo yalipita mtihani sana, na mengine yakafeli vibaya. Ajabu ni kuwa, waliopata alama za juu zaidi walitoka eneo la Waziri wa Elimu Ezekiel Machogu. Je, hiki ni kisa cha kutibuka kwa njama za kuunda jina bora au wanafunzi kutoka eneo hilo wamejaliwa akili tofauti na wengine? Huenda ni sadfa ama sivyo.


*- Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Technical University of Kenya*



**Raymond Kipkurui**

Pongezi za dhati kwa watahiniwa wote wa KCSE 2022. Nyote mlijitahidi vilivyo. Hata hivyo, utendakazi wa Wizara ya Elimu katika mitihani hiyo ya kitaifa umekuwa duni. Waziri alisisitiza "hakukuwa" na juhudi zozote za kuvuruga matokeo. Wazazi "wengi" sasa wanafikiria kupeleka watoto shule za Kaunti za Kisii na Nyamira.

*- Afisa wa Afya ya Umma*



**Mercy Meya**

Uadilifu wa matokeo ya KCSE 2022 unaibua maswali, hasa kutoka Kisii, nyumbani kwa waziri. Wanafunzi wote wanapopata alama za kuwawezesha kujiunga na chuo kikuu shule hiyo inafaa kutiliwa shaka. Wanafunzi wengi wa chuo kikuu wanahangaika kutoksababu ya matokeo feki.

*- Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Bonde la Ufa*

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "Digital Copy"

MTAZAMO WANGU



# MANDONGA ‘MTU KAZI’: KINYAGO ASIYESHINDWA

**Ndondi:** Ujuzi ni mdogo lakini uwezo wake wa kupigia debe pigano ni wa hali ya juu…Anahitaji mikebe ya ya kubingiria haraka kumwezesha kuendelea

• NA WAGA ODONGO

Ni vigumu kumwelezea raia wa Uganda Mandonga ni nani na ni kwa nini yeye ni maarufu. Ni mwanandondi asiyeweza kupigana, mpiganaji ambaye sifa zake bora huwekwa wazi kabla ya pigano. Hawataelewa, mvuto wake unaisha unapofika Busia. Kila nchi inaonekana kuwa na uwezo wa kuwa na watu mashuhuri wanaotambuliwa katika eneo lake na Mandonga ni mfano bora.

Sio tu kikwazo cha lugha. Mandonga ni mpenda mzaha kwetu sisi tunaozungumza Kiswahili. Anapojitangaza, Karimu Said hurudia jina lake la utani,“Mandonga” lenye maana ya makonde mazito na kauli mbiu yake,“Mtu Kazi”, yaani mtu wa vitendo. Lakini sifa zake ni kinyume - ni mtu wa maneno tu. Anazungumza mengi na kusema machache.

Sarakasi yake inaonekana wazi kwenye mtandao wa kijamii ambako watu huwa si makini kwa kupima maneno. Amekuwa maarufu kwa sababu anazungumza kwa kutumia maneno ya kuvutia. Anajitambulisha kwa majina ya vitu au watu wengine. Hukwepa maswali akihojiwa huku akirudia maneno yaliyozoewa.

Kauli mbiu zake hazina maana, ni kelele tu ambazo humfanya kukumbukwa. Aliendelea kusema “Mandonga Mtu Kazi”, hadi jina hilo likamea.

Hasa, nimesoma taarifa kadhaa ambapo mwanahabari husika humtaja Said kila mara akitumia jina lake la utani kama jina lake la mwisho, bila kufahamu kuwa ni jina lake la kupigana.

Said anafaa kufunza kozi ya kuvumisha bidhaa katika chuo kikuu kutokjana na uwezo wake wa kuteka hisia za watu.

Mandonga anajua kuzungumza. Anavumisha mapigano yake kwa ubora wa hali ya juu.

Kwanza kuna hali ya kupuuza wapinzani wake kitoto. Alimbatiza mpinzani wake Ali Baba Tarimo kuwa Ali “Mama”. Kisha kuna



Mwanandondi wa Tanzania Karim Mandonga akiwa jijini Nairobi mnamo Januari 13. PICHA | SILA KIPLAGAT

ngumi yenye nguvu za kiajabu ambayo pia ameibatiza.

Kila pigano lina aina mpya ya ngumi inayotokana na matukio ya kisasa. Tulikuwa na ngumi kwa jina “Peresu, Peresu” iyohusishwa na Kombe la Dunia Qatar, tulikuwa na “Ndoige” iliyosemekana kuwa isiyoepukwa siku ya Hukumu. Ilikuwa kama risasi yenye jina lako isiyoweza kuepukwa. Ingeweza kupiga kona na kukupata hata ukijaribu kuihepa. Ngumi zake zilikuwa makombora yanayosaka binadamu.

Kisha tuna “Sungunyo” ambayo ilimlenga na kumpata vizuri Daniel Wanyonyi. “Sungunyo” ilikuwa silaha iliyoundwa wakati wa vita nchini Ukraine, inayoweza kuwa jaribio lisiloruhusiwa chini ya Mkataba wa Geneva unaodhibiti matumizi ya silaha za kikemikali na kibayolojia katika maeneo ya vita.

Urusi ina aina kadhaa za silaha kali kama vile Novichok, sumu isiyo na harufu na isiyoonekana iliyopakwa ndani ya mavazi ya ndani muasi Alexei Navalny. Labda “Sungunyo” ilikuwa kitu sawa na hicho. Silaha hii ilikuwa inaingizwa Kenya kisiri kutumiwa dhidi ya mpinzani asiye na ufahamu. Kwa mtu mwingine mzaha huo ungekuwa wa kuogofya.

Vita nchini Ukraine vina dalili zote za kuashiria kuwa ulimwenguni unaelekea katika Vita vya Tatu vya Dunia bila kufahamu vikosi vya mataifa wanachama wa NATO vikiletwa kulinda Ukraine na Warusi wakitisha kutumia zana za kinuklia. Mzaha kuhusu Ukraine unavuka mipaka, lakini Mandonga aliweza kufaulu kwa kuutumia.

Hulka yake ni ya mtu domo kaya, anayejiamini kupita kiasi na mpungufu wa ujuzi; watu kama hao ni wengi Uswahilini. Ni kama Abunuwasi wa kisasa - anayejua kila kitu. Mwenye sifa za kibonzo, anayeongea kwa maringo. Sarakasi yake hiyo haingefaulu kama Mandonga angekuwa mpiganaji hodari.

Majivuno ya aliyekuwa bingwa wa ndondi Deonte Wilder yaliogofya kwa sababu kwa hakika ngumi zake zilikuwa kali. Kali zaidi. Aliposema alitarajia kuua mtu katika pigano, alitozwa faini kwa sababu alipiga kwa nguvu kiasi kwamba angesababisha kifo.

Sipendi kutazama mapigano hayo kwani hakuna ujuzi au ubunifu wa kufurahiwa. Anapenda sana kipaza sauti, ujuzi wake ni wa kuzungumza sio wa kupigana. Mapigano ya Mandonga mara nyingi huwa mfano wa maonyesho. Hakuna mtu anayeyaona kuwa mashindano halisi ya kispoti.

Tunakuja kwa maandalizi, vichekesho na sarakasi na hotuba kwa wanahabari baada ya pigano. Wakati huo, ngumi hafifu zinarushwa.

Mandonga ni maarufu licha ya kushiriki mapigano machache kuliko vidole vyake. Mchezo wa ndondi unajulikana kwa kuwakuza wapiganaji wenye rekodi hafifu. Mwanzoni unapoona dalili za wanandondi shupavu kile unachoona ni wasiovutia na waliokuwepo. Wengi wataanguka kwa kushtuliwa tu hata kabla ya kupingwa ngumi.

Mandonga ameshinda mara nne pekee, ameshindwa mara tatu na kutoka sare mara moja. Mapigano aliyopoteza yanatia hofu. Ameangushwa na kushindwa kuamka katika mapigano yote matatu aliyopoteza. Akiwa na miaka 40, wakati wake wa kung’aa unayoyoma na pia hana uwezo wa kuonyesha miondoko sawa na wapiganaji wengine walio na miaka 40.

Mandonga anacheza mchezo hatari: Ujuzi wake haufikii kiwango kinachohitajika lakini uwezo wake wa kupigia debe pigano ni bora zaidi. Anahitaji mikebe ya itakayobingiria haraka kumwezesha kuendelea. Kufikia sasa imekuwa ni kugonga na kukosa. Binafsi nina sababu ya kuchangamshwa na Mandonga. Hunifanya kupenda Kiswahili tena.

Niligundua ninatumia Kiingereza pekee katika mawasiliano. Mama yangu hunizungumzia kwa Kiingereza pekee, hivyo kufanya lugha yangu ya Mama kuwa Kiingereza. Marafiki zangu hutumia Kiingereza kwa wingi kuliko Kiswahili. Nyakati tunapotumia Kiswahili ni tunapozungumza kuhusu siasa.

*Bw Odongo ni Mhandisi Programu za Kompyuta*

***wagaodongo@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

MASOKO YA PESA

# KUFANYA PESA ZIKUTUMIKIE

**Eric Jackson na washirika wake wanasaidia watu wa kawaida kuimarisha ufahamu wao wa kifedha na kukuza utajiri kupitia jukwaa lao bunifu la uwekezaji, Hisa**

● NA EDDY ASHIOYA

Pengine kama Eric Jackson angeweza, angesimamisha wakati kusonga ili tu aweze kunusa maua ya yungiyungi kwa muda mrefu zaidi. Mkakamavu, shupavu kiasi na anayezungumza kwa upole, kama mungu mdogo wa chuma, anapasua mazungumzo kwa kicheko, akitoa hadithi hapa, mafunzo pale. Mwanzilishi huyu mwenza wa Hisa App mwenye umri wa miaka 32, ana heshima sana, huwezi kumtoa kosa kwa hilo.

Swali kubwa katika midomo linahusu ni kwa nini ametulia hivyo na zaidi ni kwa nini ana majina mawili ya Kiingereza? "Unaweza kuuliza mama yangu," anasema. "Alinipa majina mawili ya Kiingereza. Sijui ni kwa nini. Na sijawahi kuuliza." Sawa basi, nikumbushe kuuliza nambari ya simu ya mama yake. Lakini nitauliza nini, hata hivyo, safari yake kutoka kuwa Mhandisi hadi mjasiriamali.

Hisa, anasema, ilizaliwa kutokana na shida. "Tulijaribu kuwekeza ng'ambo, hasa Amerika, na tukapata ni vigumu sana. Badala ya kuvunjika moyo, tuliamua kukuza wazo hili ili kusaidia wengine kuwekeza, sio tu humu nchini, lakini pia kimataifa. Tuliamua kuunda chombo cha uwekezaji ambacho kila mtu anaweza kuabiri."

Kwa kusema sisi, bila shaka, anamaanisha mwanzilishi mwenza, ambaye pia anaitwa Eric. Eric Asuma. Ananiambia mwanzoni walikuwa Eric watatu, yeye, Eric Asuma na Eric mwingine ambaye ni mwanachama wa bodi yao ya ushauri. Kama Eric wawili ni kampuni, watatu ni jeshi. Eunice Nyawira ndiye wa mwisho katika fumbo hili, mafuta yanayofanya injini kufanya kazi.

Hisa kama kampuni sio tu jukwaa la uwekezaji. Watumiaji wanaweza kuchagua wanachotaka kutoka shughuli tofauti: iwe ni habari za soko la moja kwa moja, kujifunza utaalamu, kufuatilia podcast zao pendwa za kifedha na uwekezaji, na mahojiano na wataalamu.

"Katika Hisa, tunajenga muundo msingi wa uwekezaji usio na mipaka Afrika kupitia uwekezaji mdogo. Chini ya asilimia moja ya watu katika Afrika chini ya Sahara wanawekeza katika masoko ya hisa, hasa kutokana na ukosefu wa ufikiaji, kutofahamu vyema, ukosefu wa Matoleo ya Hisa kwa Umma (IPO) na pia viwango vya chini vya hisa za kuuzwa kupata pesa," anasema Erick Asuma.

Hisa sio biashara ya kwanza ya kina Eric na Eunice. Wanaendesha pia Kenyan Wallstreet, jarida la mtandaoni sawa na New York Wall Street Journal. Kuweza kufanikiwa kuendesha kampuni mbili kwa wakati mmoja, anasema, ni kutaka kupasha habari kila siku. "Katika Kenyan Wallstreet, tunakufahamisha kinachoendelea katika ulimwengu wa biashara na fedha. Katika Hisa tunasaidia watu kuwekeza vyema na kukuza utajiri wao na pia kuimarisha ufahamu wa masuala ya kifedha. Tunatumia Kenyan Wallstreet kutoa habari, podcasts na matini kuhusu data za kifedha. Unapoelewa, unatumia ufahamu huo kuwekeza, kupitia Hisa. Ni pande mbili za sarafu moja."

Kuhusu watumiaji, kuna wapatao 18,000 wanaonunua na kuuza kupitia Hisa. Lakini Er-



Eric Jackson ndiye mwanzilishi wa apu ya Hisa, inayowezesha watu wa kawaida kuwekeza pesa zao na kupata faida. PICHA I MAKTABA

Nation Media Group Digital Copy




**Eric Jackson akiwa na mameneja wakuu wa Soko la Hisa la Nairobi wakiongozwa na Afisa Mkuu Mtendaji Geoffrey Odundo wakati wa kuzinduliwa kwa apu ya Hisa.** PICHA | MAKTABA

ic ana lengo kubwa: "Kufikia Mei 1 [2023], tunatarajia kufikisha watumiaji 200,000 katika apu yetu." Kufikia sasa, zaidi ya dola milioni moja zimeuzwa kupitia jukwaa hili.

Lakini apu ni biashara ghali mno. Wanatengeneza pesa vipi? "Waanzilishi wenza wetu walisaidia biashara kwa pesa zao, kutoka 2020. Tulikusanya pesa kuendesha biashara mwanzoni. Kwa sasa tunatafuta pesa kupata dola milioni moja kukamilisha bidhaa hii na ituruhusu kuimarika." Kuhusu kutengeneza pesa, anasema, Hisa hutoza ada ya asilimia moja ya kila biashara. "Lengo letu ni kupata faida ndani ya miezi 18."

Changamoto iliyopo, anasema, hawakui haraka walivyotaka, kufikia watu wengi zaidi na kupanuka hadi masoko mengine. "Hatuwezi kukua haraka hivyo kwa sababu tunahitaji kuwa na uwekezaji mkubwa. Tunakua haraka, lakini sio vile tunataka."

Akitazama nyuma, kuna matukio ambayo yalimsukuma hadi kufika alipo leo? "Mimi ni mhandisi wa stima, lakini nilivutiwa na uundaji wa programu. Nilitanganama na kompyuta mara ya kwanza nikiwa shule ya upili. Kitu cha kushangaza ni kuwa niliunda mfumo wa mtandao wa kusimamia mabweni kwa Chuo Kikuu cha Moi ambapo wanafunzi walikuwa wakiomba vyumba wakiwa nyumbani. Hiyo ilipunguza muda wa kutafuta chumba cha kulala chuoni."

Huenda kuwepo kwake katika ujasiriamali haukuanza siku hiyo - lakini ulikuwa umepangwa. Je amejifunza nini kuhusu tabia za Wakenya na pesa? Ukweli kuwa tunafanya bidii kupata pesa lakini hatufanyi juhudi zozote kuelewa jinsi ya kutumia pesa vyema. Kwa maneno mwengine, tunafanya bidii kupata pesa lakini pesa hazitusaidii. "Na, ndio, Wakenya wanapenda njia za mkato."

"Hii ndiyo sababu katika Hisa, tunatafuta njia endelevu za kupata faida. Hii inaelezea ni kwa nini soko la hisa ni mojawapo ya njia za kuunda utajiri." Haya yote ni kusema kuwa kama mjinga Charles Ponzi angekuwa anaishi Kenya, angekuwa tajiri akijenga mipango yake ya piramidi. Tapeli ni tapeli tu.

Hata hivyo, ufanisi wake umepatikana kwa gharama. Hasa kwa sababu ana familia changa.

"Nina binti na wavulana wawili ambao nimegundua sijapata muda wa kutosha kuwa nao. Nimejifunza zaidi kudhibiti hali na kutambua kuwa kuna kazi na pia familia, na ukipoteza wakati, huwezi kuupata tena."

Je, amekuwa na shughuli nyingi akitafuta pesa hadi akasahau ana maisha? Pengine. Kwa kipimo, hangekuwa alipo kama hangeghairamika, lakini kwa kuwa alipenda kwa kifupi, hisia za kupoteza zilikuwa nyingi.

Eric ananiambia kuwa pesa sio lazima ziwe mbaya. Ninamwambia anahubiria wanaoamini ni mbaya. Alilelewa katika mazingira ambayo alifunzwa kuchukia pesa. "Pesa si lazima ziwe mbaya; ni jinsi unavyozitumia kuleta mabadiliko na kukuza utajiri. Ni njia ya kutimiza lengo fulani." Ninamkumbusha kuhusu hekaya ya sungura mjanja, ambapo sungura anajua hawezi kufikia matunda, na katika juhudi za kuokoa heshima yake na kuponya nafsi yake, sungura anasema matunda hayo hata hayajaiva, kwa hivyo hakuwa akiyataka.

Tofauti na sungura, yeye, Eric anatambua kuwa anakabiliana na pambano kubwa zaidi kwa binadamu: kusawazisha azima na ukweli; kwamba unaweza kuwa na mitazamo miwili inayokinzana katika akili yako; ukweli kwamba kila siku lazima uone mabadiliko lakini unaweza kuyaona kwa muda; ukiwa na njaa na mwenye azma, lakini pia kwa kutojitesa sana kwa kuwa vitu vizuri vinachukua muda.

Kuhusu suala hilo, je mambo yamekuwa alivyotarajia akiwa na umri wa miaka 32? "Nafurahia kazi na hutaka kuwa mahali ambapo ninaridhika na ninachofanya. Ni lazima kila wakati uwe na njaa na azma. Nimechukua ile njia ndefu lakini nafurahia nilipo."

Anasema yuko katika msimu wa maisha yake ambao anatosheka na jinsi alivyo. Kujifunza kuacha mambo na kuacha yajiendeshe. Hata mfalme hawezi kusimamisha jua, ndivyo anavyoamini.

***eddieashioya@gmail.com***
*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

## MAELEZO

- Hisa ina mfumo wa uwekezaji mdogo wa B2B unaoruhusu kampuni zingine za teknolojia za fedha, benki na kampuni za mawasiliano ya simu kutumia muundomsingi na uzingatiaji wake wa udhibiti kwa uwekezaji kama hisa, ETFs au hazina za fedha, sawa na apu ya simu za mkono ya B2C ambayo inaruhusu wawekezaji wa rejareja kununua hisa- za humu nchini na kote duniani - na pia ETFs na REITs.
- Hisa imeshirikiana na Faida Investment Bank, kuhifadhi pesa za wawekezaji. Hii inamaanisha kuwa mambo yakienda vibaya katika Hisa, wawekezaji wanaweza kufidiwa.
- Hisa ilikuwa apu ya kwanza ya simu kupata idhini kutoka kwa Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Soko la Hisa la Nairobi (NSE) kuwezesha uwekezaji wa hisa zilizopungua. Aina hii ya uwekezaji inaruhusu watu kununua chini ya hisa kamili, na kufungua ufikiaji wa hisa ambao ingekuwa vigumu kumudu kutokana na bei ya juu.
- Ingawa kwa sasa inahudumu Kenya- Hisa tayari imetia saini ushirikiano Rwanda na Tanzania na inanuia kupanua shughuli zake katika nchi hizi, sawa na Zambia, katika nusu ya kwanza ya 2023.
- Apu ya Hisa ilizinduliwa rasmi kwa biashara katika NSE mnamo Novemba 2022 baada ya muda wa kufanyiwa majaribio wa miezi 10. Hisa inapatikana katika iOS AppStore, Google Playstore.

Nation Media Group "Digital Copy"

AFYA NA LISHE

# MAISHA YA MWILI TIMAMU

**Mwangi anapokunja mikono yake, unachoona ni misuli iliyokonda na migumu. Amejitolea kwa miaka 20 iliyopita kuhamasisha wateja kuhusu maisha yenye afya**



Kevin Mwangi (kushoto) wa Rollin Total Fitness na kocha Stephen Adika jijini Nairobi, Desemba 20 mwaka jana. PICHA I LUCY WANJIRU

• NA SINDA MATIKO

Um, sawa…. Je, kila mtu anapaswa kula chakula gani kudumisha ujana hivi?

Ninapokutana naye, Kevin Mwangi anatoka kwenye karamu ndogo aliyofanyia familia yake. "Ilikuwa hafla ndogo tu ya kifamilia kusherehekea maisha," anasema huku akitabasamu.

'Mwas' au 'Kevo' kama wengi wanavyomuita, ndio ametimiza umri wa miaka 40. Kwa kumtazama, Mwangi anaonekana kuwa mtu mwenye umri wa kati ya miaka 20 na 30.

Huyu si mtu wa aliye na umri wa miaka 40. Ni vigumu kuona mkunjo kwenye uso wake, wala mstari mwembamba chini ya macho yake, sifa kuu ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 40.

Mashavu ya Mwangi hayana ulegevu wa mikunjo ama mfano wa ngozi bali ni thabiti. Ingawa watu wengi siku hizi hujaribu kupunguza kasi ya kuzeeka kwa kutumia bidhaa za kutunza ngozi, Mwangi ambaye ni mshauri wa mazoezi ya viungo, hachukui njia za mkato. Akiwa na uzito wa kilo 67, mwili wake mdogo unakaa vizuri. Yeye huamka kila siku saa kumi na nusu asubuhi ili kupata mlo wake wa kwanza wa siku na kupanga vipindi vyake vya mazoezi. Kufikia saa mbili asubuhi yuko kwenye ofisi yake katika Valley View, Parklands, akihudumia wateja walio na changamoto mbalimbali za afya ya viungo.

Mwangi anapokunja mikono yake, unachoona ni misuli migumu na iliyokonda, thibitisho la miaka mingi ya shughuli za mazoezi. Kifua chake kinatutumka nje huku misuli yake ya miraba sita ikisukuma fulana nyeusi na nyembamba anayovaa siku hii.

Tunapoanza kuongea, anaanza kusikika zaidi kama mwimbaji wa 'Forever a Fly Girl'

Jennifer Lopez (J-Lo), mwenye umri wa miaka 53, ambaye amedumisha ujana kwa miaka mingi. "Uthibitisho ni muhimu. Kuweka mawazo chanya ni muhimu sawa tu na lishe na mazoezi. Mimi ni kijana kila wakati. Ninajiambia kuwa kila siku umri uko akilini mwako," aliwahi kusema J-Lo kwenye mahojiano. Mwangi ana maoni sawa.

Kwa miaka 20 iliyopita, mtaalamu huyo wa mazoezi ya viungo amejitolea maisha yake kuelimisha, kuwezesha na kuwatia moyo wateja kuelekea kuishi maisha yenye afya na viungo timamu, na kuelewa lishe na sayansi inayoleta mambo hayo.

"Hiyo ndiyo sababu pekee ya watu wengi kusema ninaonekana mwenye umri mdogo kuliko nilionaoni. Nimekuwa nikiishi maisha mazoezi tangu nikiwa kijana," anasema.

Akiwa katika shule ya upili, Mwangi alinenepa lakini hata hakumkaribia ndugu yake mdogo aliyekuwa msimamizi wa jumba la chakula kutokana na mwili wake mkubwa.

"Kwa sababu nilikuwa mkubwa wake kwa umri, nilichekwa shuleni. Ndugu yangu alikuwa akinyanyua uzito lakini mimi nilipenda muziki, lakini kutokana na kuchekwa niliamua kujiunga na mazoezi ya viungo na kujenga misuli kwa kunyanyua uzito. Nilikuwa na bahati kwamba baba yangu alikuwa na jumba dogo la mazoezi, Rollin, mtaa wa Kayole. Bado lipo hadi sasa."

Safari ya kupunguza uzito na kuonekana mzuri iligeuka kuwa uraibu na hatimaye ikawa biashara.

"Baada ya kumaliza Kidato cha Nne 1999, baba yangu alinipa jukumu la kusimamia jumba lake la mazoezi. Haikuwa biashara yenye faida wakati huo. Kulikuwa na dhana nyingi sana potovu kuhusu kumbi za mazoezi wakati huo kwa sababu wateja wengi walikuwa wa watu wa kudumisha usalama na nidhamu kwenye baa na walinzi.

Leo hii, biashara ya mazoezi ya viungo imenoga na watu kama Mwangi wanapata faida kubwa kutokana nayo. Amekuwa akisimamia Rollin Total Fitness kwa zaidi ya mwongo mmoja sasa. Kampuni hiyo huagiza na kuuza virutubisho huku pia ikitoa huduma za tathmini ya mwili na mashauri kuhusu lishe.

"Nilipoanza kusimamia jumba la mazoezi la baba yangu, niligundua kuwa changamoto kubwa ilikuwa kudumisha wateja. Kama wangefanya mazoezi na kukosa kujenga misuli wangetoweka." Baada ya kufanya vyema katika masomo ya sayansi, Mwangi alikuwa na ufahamu mzuri wa maumbile ya binadamu. Alianza kutafiti matumizi ya virutubisho.

"Hapakuwa na habari nyingi wakati huo. Nilianza kwa kuuza bidhaa mbili ambazo niliziele wa vizuri, moja ikiwa Creatine." Si

Nation Media Group "Digital Copy"




Kevin Mwangi (kushoto) na Bw Physique (2017-2018) Joseph Oyatta katika Rollin Total Fitness jini Nairobi. PICHA I MAKTABA

watu wengi waliokuwa na habari kuhusu virutubisho na Mwangi alilazimika kufanya mengi ya kuongeza ufahamu.

"Ilibidi kwanza nielimishe watu kwa sababu wengi walidhani kuwa dawa hizo ni kokeni kwa sababu zilikuwa poda nyeupe. Nilihakikisha wanaelewa kuwa hicho kilikuwa chakula cha kusaidia kujenga misuli yao," anakumbuka.

Pole pole, wateja wachache wenye shaka waliamua kutumiwa kwa majaribio walianza kuongeza misuli na habari hizo zikaenea sana. Wateja waliongezeka na mahitaji ya bidhaa pia yakaongezeka. Lakini Mwangi bado hakuwa akipata faida yoyote kutokana na biashara hiyo.

"Virutubisho vimekuwa ghali na si watu wengi wangeweza kumudu wakati huo. Nilinunua kwa bei ya jumla lakini mwishowe sikupata faida yoyote kwa sababu niliuza kwa vijikoalivyohitaji mtu au kwa kidonge, kulingana na bidhaa. Nilipata hasara kila wakati."

Kulingana na bei ya sasa katika soko, virutubisho muhimu vya kabla na baada ya mazoezi vinagharimu angalao Sh10,000. Virutubisho vya protini bora hugharimu kati ya 6,500 na Sh11,000 kwa pakiti ya kilo moja na nusu.

Lakini hata bila kupata faida yoyote, Mwangi aliamua kudumisha wateja wake kwenye ukumbi wa mazoezi na kuongeza idadi yao.

"Nililazimika kuendelea kufanya biashara bila kupata faida yoyote ya maana kwa sababu nilitambua kuwa nilikuwa najenga uaminifu hasa kwa wajenzi misuli ambao nilikuwa nikitangamana nao."

Huku idadi ya wateja wake ikiongezeka kwa haraka na bila pesa za kutosha kuanzisha biashara, Mwangi alibuni wazo.

"Wakati huo, karibu kila aliyekuwa akifanya mazoezi ya mwili Nairobi alinijua kwa sababu nilikuwa nikitembea na mfuko wa nikiwauzia virutubisho kwa kiasi kidogo. Walikuwa wameniamini haraka kuliko nilivyotarajia. Nilianza kutambulishwa kwa wauzaji virutubisho nje ya nchi." Huku wajenzi wengi wa mwili na wateja wengine mashuhuri wakitangaza biashara yake, wasambazaji walianza kumletea virutubisho vya thamani ya mamilioni ya pesa.

"Kwa sababu ya uaminifu niliojenga, wasambazaji wengi walinichagua kuwa wakala wao. Wangeniletea bidhaa na kuniruhusu niuze kwa niaba yao. Kisha nililipwa kwa kuttokana na mauzo."

Mwangi alianzisha kituo cha kujengea misuli cha Rolling Total Fitness wakati fulani

mwaka wa 2011 na kuanza kwa kupokea bidhaa kwa mkopo."Uaminifu umekuwa kila kitu kwa biashara yangu kwa sababu wasambazaji hawa wangeniletea bidhaa na kuniruhusu niziuze kwa mkopo na kuzilipa baadaye au kwa awamu. Hivyo ndivyo nilivyoweza kujenga biashara kwa kuweka mbele maslahi ya wateja badala ya pesa," anasema Mwangi.

Katika miaka ya hivi majuzi, kumekuwa na ongezeko la viwanja vya mazoezi ya mwili vinavyochipuka katika miji mikubwa huku wakazi wengi wa mijini wakiendelea kuhangaika zaidi kuhusu hali zao za kiafya.

Kile ambacho hali hiyo imefanya ni kupanua biashara ya sekta ya mazoezi ya mwili kuwa himaya ya mamilioni ya pesa kulingana na uchunguzi wa Mwangi.

"Bado ni mapema lakini siku zijazo zinaonekana kuwa nzuri. Nimeona ongezeko la ghafla la matamanio ya utimamu wa mwili Nairobi, Eldoret na Mombasa.

Hii ndiyo miji mikuu inayosaidia biashara ya mazoezi ya mwili nchini Kenya kwa sasa. Kuna wanariadha wengi katika miji hii na kuongezeka kwa watu wanaojiunga na kumbi za mazoezi ya mwili. Kwa hivyo kumbi za mazoezi ya mwili pia zinaongezeka Kisha mazoezi ya viungo pia yanaongezeka." Wateja wa Mwangi kwa sasa wanajumuisha watu mashuhuri, wanasiasa na wafanyabiashara maarufu.

"Kwa wanasiasa, wanariadha, na wafanyabiashara singependa kuwataja kwa majina kwa sababu waliomba usiri wa mteja. Kuhusu watu mashuhuri, baadhi yao ni KRG The Don, Khaligraph Jones, Redsan na Daniel Ndambuki maarufu kama Churchill miongoni

mwa wengine.

*tmatiko@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

## UONGOZI MPYA

*Na J. Nyaganyagah*


jnyaga@ke.nationmedia.com

### UWEZO WA MWANAMKE



ROSEMARY NAMBOOZE WA UGANDA NI MMOJA WA WANACHAMA SITA WAHISANI DUNIA NZIMA AMBAO WAMETAMBULIWA KUWA 'WAHISANI KWA VITENDO: BINGWA WA UJUMUISHAJI KWA KUELIMISHA NA KULEA WATOTO WALEMAVU KIAKILI'. MWENYEWE AKIWA MAMA AMBAYE MTOTO WAKE ANA ULEMAVU WA AINA HIYO, NAMBOOZE ANASEMA ALIGUNDUA UKOSEFU WA MSAADA WA KIJAMII KWA WATOTO WENYE ULEMAVU NA UNYANYAPAA UNAOWAKABILI. KWA HIVYO ALIANZISHA SHIRIKA LA ANGEL'S CENTRE KWA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM MNAMO 2012, LINALOTOA ELIMU NA HUDUMA ZA MATIBABU KWA WATOTO HAO PAMOJA NA KUSAIDIA WAHUDUMU NA WALIMU WAO.

### NYOTA WA WIKI



MASHABIKI WA MCHEZO WA RAGA KOTE DUNIANI WIKI ILIYOPITA WALIMSIFIA MCHEZAJI MAARUFU WA KENYA SEVENS COLLINS INJERA, WAKISEMA SIFA ZAKE ZITADUMU MILELE.

INJERA, 36, AMBAYE KWA SASA NDIYE WA PILI KWA KUFUNGA MABAO KATIKA RAGA YA SEVENS NA MCHEZAJI BORA WA FAINALI YA 2016 NCHINI SINGAPORE, ALISTAAFU BAADA YA UFANISI MKUBWA WA MIONGO MIWILI KATIKA MCHEZO HUO.

INJERA ALISEMA IMEKUWA VIGUMU KWAKE BAADA YA MIAKA 17 YA DAMU, JASHO NA MACHOZI KUTOKA KATIKA MCHEZO HUO MZURI AMBAO UMEMFAA SANA MAISHANI. TUNAKUTAMBUA, COLLINS, NA TUNAKUTAKIA KILA LA HERI KATIKA MIAKA IJAYO.

Nation Media Group "ePaper Copy"

maoni




■ Wanasiasa hawafai kulazimisha Wakenya mipango yao ya kujifaidi iliyofikiwa faraghani

# Wakenya wamechoshwa na mikataba ya siri



KWENDO
OPANGA

Kwa nini kuna gumzo kuhusu 'handisheki'? Moja, kwa sababu siasa za Kenya hafanya watu kuwa marafiki wa ajabu. Pili, kwa sababu anachokwambia mwanasiasa mchana sicho atakachosema usiku. Tatu, usaliti hubuni na kuvunja vyama vya kisiasa na, nne, viongozi huwa hawana misimamo.

Kwa hivyo, nilichotaja mwaka wa 2016 hadi 2020, kuwa shida ya kila miaka mitano, ni kwamba sisi, watu, tunakukimbia kwenye vituo vya kupigia kura. Tunangoja kwa subira kwenye foleni, vitambulisho vikiwa mkononi au mfukoni, kisha, tunapiga kura na kwenda nyumbani au kazini au kwingineko kungojea matokeo.

Kisha, ghafla bin vuu, hatuwezi kuhesabu. Kwa hivyo, kura ya mtu haina maana na, kwa ghafla hiyo, mwamuzi wa kura anaivuruga.

Mnamo Desemba 2007, dalili zote zilionyesha kuwa Bw Raila Odinga wa Orange Democratic Movement (ODM) angetangazwa kuwa rais dhidi ya rais aliyekuwa mamlakani, Mwai Kibaki.

Kisha kura za kimiujiza kutoka Tharaka Nithi zikamimika na kuongeza hesabu na marehemu Samuel Kivuitu akasema kuwa angetangaza matokeo hata kama ingemaanisha kufanya hivyo kutoka kwa meli ya kivita.

Miongoni mwa watu waliokuwa katika jumba la Kenyatta International Convention Centre ambao walikuwa wameamua kuzuia tangazo la kuchaguliwa tena kwa Kibaki kama urais ni William Ruto, ambaye alikuwa amechaguliwa tena kuwa Mbunge wa Eldoret Kaskazini.

Meli ya vita au la, Ruto aliamini kwamba Odinga, wala si Kibaki, ndiye aliyechaguliwa kuwa Rais. Aliyekuwa na msimamo mkali kama Ruto katika kambi ya Kibaki ni Martha Karua. Hatimaye Ruto alikasirika sana Odinga alipoamua kuingia kwenye mazungumzo ambayo yaliishia kwenye mpango wa kugawana mamlaka kati ya Chama cha Kibaki cha Party of National Unity na ODM. Kwa upande wake, Karua alishikilia kuwa ODM ilishindwa katika uchaguzi lakini ikatumia kifua kuingia serikalini.

Ruto na Odinga walitofautiana baadaaye alipokuwa Waziri Mkuu na akamfuta kazi kutoka kwa wadhifa wa Waziri wa Kilimo.

Katika kilele cha makabiliano yao, Odinga aliuliza kwa kejeli, Ruto ni nani? Alikuwa akisema kuwa yeye na Ruto si wa ligi moja kisiasa. Mnamo 2013, Ruto aliteuliwa kuwa Naibu Rais, kupitia Katiba aliyopinga na ambayo Odinga aliunga mkono.

Mambo yalikuwa yamegeuka. Odinga alidai alinyang'anywa ushindi wake. Mahakama ya Upeo haikumfaa. Ujumbe wake wa mwisho kuhusu uchaguzi huo ulikuwa kwamba Mahakama ya Upeo iliyoongozwa na Jaji Mkuu Willy Mutunga ilikuwa bandia. Lakini miaka mitano baadaye, Jaji Mkuu David Maraga alipotoa uamuzi wa kumuunga mkono Odinga baada ya uchaguzi mwingine uliokumbwa na utata, Odinga alisusia marudio ya uchaguzi aliyoamuru.

Kwa nini? Kwa sababu alisema, mwamuzi wa uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), bado ingeiba kura kumpendelea Uhuru. Lakini mnamo 2022, ni tume hiyo hiyo ilikuwepo na Odinga anasema aliyekuwa mwenyekiti wake Wafula Chebukati alibadilisha maamuzi ya wananchi kwa kuiba kura zake na kumpa Ruto.

Na, kuanzia leo, Odinga na washirika wake wamerudi barabarani.

Na hiyo ndiyo sababu Ruto na washirika wake wanalalamika kuwa Odinga anatishia kuongoza maandamano ili kulazimisha serikali kufanya mazungumzo naye, kama alivyofanya na Rais Kenyatta mnamo 2018, na kuingia serikalini. Bila shaka, Odinga na washirika wake wanasema suala hapa ni kuwa Ruto anajaribu kubuni IEBC itakayosimamia uchaguzi ujao, kwa kuwa Chebukati amestaafu.

Muda mrefu kabla ya 'handisheki' ya Machi 2018, nilikuwa na hoja kwamba hakufai kuwa na mikataba ya kisiasa kwa sababu hii ni mikataba ya siri kati ya wanasiasa nchini Kenya, wala si kandarasi kati ya Wakenya kuhusu Kenya. IEBC haipaswi kubuniwa kwa ajili ya wanasiasa, wala wanasiasa hawapaswi kulazimisha Wakenya mikataba yao ya kujinufaisha iliyofikiwa kisiri maofisini.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

maoni

■ Amri hiyo, kama inaweza kuitwa hivyo, ilikuwa isiyoweza kutekelezwa, haramu na kinyume cha katiba

# Bwana Rais, usiguse chupa yangu



MACHARIA GAITHO

Rais William Ruto anafahamika kuwa mtu asiyekunywa pombe, na hiyo ni haki yake. Pia ameelezea wasiwasi wake kuhusu ulevi wa kupindukia, hasa miongoni mwa vijana ambao katika baadhi ya maeneo nchini wamegeuka wajinga.

Kuna uwezekano kuwa kupanda kwa Ruto hadi kiti hicho kikuu kisiasa kumewezeshwa, kwa njia moja, na hali kuwa hagusi pombe. Ni mwenye nidhamu, lengo, mchapa kazi na amebarikiwa kwa msukumo wa kufuata malengo yake.

Kama Rais, anapaswa kuwa na wasiwasi kuwa wengi wa watu anaoongoza wanaharibu maisha yao kwa kutekwa na kinywaji hicho cha kishetani.

Ulevi kupindukia unaharibu sio tu watu binafsi, bali familia, jamii, mfumo mpana wa kijamii na pia kuathiri vibaya uchumi wa kitaifa.

Watoto huachwa bila kuhudumiwa na kushikwa na kiwewe wazazi wao wakinywa pombe zaidi. Pesa za familia huishia kwenye baa na watoto kunyimwa upendo na mwongozo wa wazazi na wajibu wa kuwapa elimu, mavazi, huduma za afya na nyumba.

Ulevi huongeza mzigo kwa mifumo ya afya rasilimali haba zinapoelekezwa kushughulikia madhara yanayotokana na unywaji pombe.

Malengo ya maendeleo huathirika wanaopaswa kufanyakazi, kutoa huduma, bidhaa na maarifa wakizama katika pombe.

Hasa, unywaji pombe ni tatizo la kitaifa na hapa lazima tukomeshe kabisa upuzi huo ambao kwa kiwango kikubwa ni shida ya kipekee katika eneo la Katikati mwa Kenya.

Hakika kama kuna jamii ambayo ulevi umekuwa jangaa, ukiathiri wanaume kwa wanawake wa kila umri, asili yao, hali yao ya kiuchumi na kijamii, ni eneo la Rais Ruto mwenyewe la Rift Valley.

Hatua inafaa kuchukuliwa na ni wajibu wa Rais kuongoza serikali yake katika kuchukua hatua hiyo.

Hata hivyo, hali kwamba tuna shida ya ulevi isiwe sababu ya Ruto kujaribu kulazimisha hulka yake ya kutokunywa pombe kwa Wakenya wengine.

Anaweza kuendelea kupata kikombe chake cha chai moto bila kutumia vibaya mamlaka yake ya urais kulazimisha kila mtu kuachana kinywaji wanachopenda. Kwa hivyo, agizo lake la juzi la kupunguza baa Kenya hadi moja katika kila eneobunge halikufaa.

Linaweza kufananishwa na maagizo ya kiholela ya nyakati za utawala wa Moi na halitaleta faida yoyote isipokuwa kutoa mwanya kwa maafisa wa polisi na maafisa wa utawala kuendeleza ufisadi.

Amri hiyo, kama inaweza kuitwa hivyo, ilikuwa isiyoweza kutekelezwa, haramu, kinyume cha katiba na linaingilia mamlaka na majukumu ya serikali za kaunti. Pia ni mfano mzuri wa unafiki uliokolea katika kila ngazi ya utawala mbaya wa Kenya Kwanza.

Kwa upande mmoja, tunajifanya kupambana na ulevi kwa kufunga baa. Lakini kwa upande mwingine, tunaunga mkono na kuwasifu watengenezaji pombe, wakiwemo waliopata umaarufu kwa kukwepa kulipa ushuru. Tunawataja kuwa wafanyabiashara wazalendo ambao hawafai kuulizwa kulipa malimbikizi ya ushuru wanayodaiwa.

Haya ni mawazo ya aina gani? Kama kweli watengenezaji pombe ni wadau muhimu katika uchumi, waajiri wakubwa na wachangiaji wa mapato ya serikali, mbona tuwalemaze kwa kufunga vituo vya kuuza na kusambaza bidhaa wanazotengeneza?

Kamwe siungi mkono ulevi wa kupindukia, utengenezaji na unywajiwa pombe haramu zenye madhara, kuwe=po kwa baa zilizo na kilele karibu na shule au maeneo ya makao. Lakini ninaelezea tu unafiki na madhara ya maagizo ya kisera yanayotolewa baada ya fikra finyu. Napenda pombe yangu. Ni kinywaji kizuri cha kirafiki kinachoniwezesha kutangamana na watu na ambacho napendelea kubugia karibu na nyumbani kwangu ili niweze kufika kwa urahisi kwa sababu sitaki kuendesha gari mbali nikiwa mlevi. Nitakuwa wa kwanza kuungama kuwa, mara nyingi, ninaweza kunywa kupita kiasi. Nilifanya hivyo mara nyingi enzi za ujana wangu lakini sidhani kimeniharibu.

**Ulevi kupindukia unaharibu sio tu watu binafsi, bali familia, jamii, mfumo mpana wa kijamii na pia kuathiri vibaya uchumi wa kitaifa. Watoto huachwa bila kuhudumiwa na kushikwa na kiwewe wazazi wao wakinywa pombe zaidi. Pesa za familia huishia kwenye baa na watoto kunyimwa upendo na mwongozo wa wazazi na wajibu wa kuwapa elimu, mavazi, huduma za afya na nyumba. Ulevi huongeza mzigo kwa mifumo ya afya rasilimali haba zinapoelekezwa kushughulikia madhara yanayotokana na unywaji pombe.**

Imebainika kuwa jinsi serikali inavyozidi kupiga marufuku pombe, ndivyo biashara hiyo inavyoendeshwa kisiri na kudhibitiwa na wahalifu.

Kufungwa kwa baa zenye leseni kutachangia kuzuka kwa baa nyingi haramu ambazo zitauza pombe haramu na hatari na kusababisha madhara kote nchini.

Kwa njia zote tudhibiti, kusimamia na kutoza ushuru, lakini tupinge jaribio la kulazimishia watu wengine maisha yetu binafsi ya kijamii au miegemeo yetu ya kidini.

Mbali na hatua zilisizosuluhisha shida hiyo, tunafaa pia kujiuliza ni kwa nini watu wengi nchini wanageuka watumwa wa ulevi, ukiwemo wa miraa, muguka, bangi, kokeni na vitu vingine vinavyoharibu akili.

Viongozi wetu wakijichunguza, watagundua wao ni sehemu ya shida hiyo. Na hatua yao ya kujionyesha kuwa wacha Mungu haitasuluhisha chochote.

Shida ni hali ya watu kupoteza matumaini, kuhisi kutengwa, umaskini, kukosa ajira, kutotendewa haki kijamii na kiuchumi na changamoto zote ambazo serikali imekataa kusuluhisha.

Vijana wetu wanaambiwa wafanye kazi kwa bidii na waishi maisha yenye maadili lakini wanayoona kila siku ni viongozi wanaotoa ahadi za uongo, wakiishi maisha ya utajiri yanayogharamiwa na umma na wanaopora pesa za umma bila hofu ya kukamatwa.

Mwanamume au mwanamke mchanga anayeiba kuku au paketi ya unga kutokana na kukata tamaa maishani atafungwa jela miaka mingi kama hatauawa barabarani ilhali tajiri anayeiba kutoka kwa Kampuni ya Stima, Kampuni ya Mafuta, Hazina ya Kaunti au taasisi nyingine za umma anasifiwa na kupandishwa cheo bora tu anaunga mkono walio mamlakani. Bwana Rais, unahitaji kinywaji. Kitakufungua macho.

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

■ NI MKENYA WA KWANZA KUTAMBULIWA NA FIJI KWA UMAARUFU WA RAGA

# SHUJAA WA KWELI WA RAGA

• NA BRIAN WASUNA

Gwiji wa mchezo wa raga, hazina ya kitaifa na nembo ya ulimwengu. Na pengine zaidi.

Baada ya miaka 17, tuzo nyingi za timu nyingi na za kibinafsi, nyota maarufu wa raga Collins Injera amestaafu mojawapo ya spoti inayohusu mtangusano zaidi.

Jinsi tu alivyokuwa wakati wake katika mchezo huo, kustaafu kwa Injera ni spesheli. Kwanza, ameacha kumbukumbu ambayo mamilioni watajaribu kuiga katika siku zijazo. Na pia, kunakumbusha kila mtu kuwa kila kitu kina mwisho wake.


"Atakuwa kiongozi wa dunia. Ujuzi wake wa uongozi unaonyesha amekomaa zaidi. Uwanjani, ni hodari. . ." aliyekuwa kocha mkuu wa Kenya Sevens Mitch Ocholla alisema kumhusu Injera mnamo 2016, kufuatia uteuzi wa kipekee wa timu ya taifa na mmoja wa wachezaji wake muhimu.

Injera anapoondoka uwanjani, anaanza kazi katika Umoja wa Mataifa kama Mshirika wa Ubora wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Akiwa tayari mashuhuri katika spoti duniani, jukumu hilo jipya linaweza kuwa mwanzo wa kuiga mfano wake huo katika sekta ya masuala ya ubinadamu.

Mnamo Januari 11, Injera alikuwa Mkenya wa kwanza na wa pili Afrika, baada ya mzaliwa wa Johannesburg- Brian Habana, kutambuliwa nchini Fiji katika Orodha ya Wachezaji Mashuhuri wa Raga maarufu kama Rugby Town Walk of Fame. Rugby Town Walk of Fame ni mpango wa heshima katika mji wa Fiji wa Sigatoka. Mpango huo hutambua wachezaji shupavu wa raga duniani ambao wametoa mchango mkubwa katika mchezo huo.

Waliowahi kujumulishwa katika mpango huo ni David Campese (Australia), Waisale Serevi (Fiji), Jonah Lomu (New Zealand), Viliame Satala (Fiji), Ben Gollings (England), Karl Te Nana (New Zealand) na Lote Tuqiri (Australia), Habana na timu ya raga ya Fiji Sevens iliyoshinda dhahabu katika michezo ya Olimpiki mnamo 2016.

## Injera astaafu baada ya mechi 279 za Sevens, Kombe la Dunia mara nne, mechi 424 za mashindano 83 ya kimataifa - nyingi zaidi kuchezwa na Mkenya - na Olimpiki mara mbili



Collins Injera wakati wa Safari Sevens katika uwanja wa RFUEA mnamo 2008. CHRIS OMOLLO I NATION

Sawa tu na wachezaji wengi wa raga wa kizazi chake, aliingia katika mchezo huo kwa bahati. Injera, ambaye alikua akicheza soka, alianza kujaribu mchezo huo alipojiunga na Shule ya Upili ya Vihiga.

Baada ya kumaliza Kidato cha Nne Vihiga mnamo 2004 akiwa tineja, Injera alimfuata kaka yake, Humphrey Kayange, gwiji mwingine wa mchezo huo, kujiunga na klabu ya raga ya jeshi Ulinzi RFC.

Kama wakuu wa jeshi wangejua kile ambacho Kayange, Injera na wachezaji wengine kama Dennis Mwanja wangebadilika kuwa, pengine hawangevunja Ulinzi RFC mnamo 2005.

Lakini walikubali hali hiyo! Injera na Kayange walijiunga na Mwamba RFC, ambapo mara moja walikuwa viungo muhimu vya klabu hiyo iliyoshikilia nafasi spesheli katika historia ya raga Kenya. Katika shindano la wachezaji saba kila upande, Injera na Kayange walikuwa wa kutegemewa. Walikuwa wa ajabu kutazama na mmoja wao angeunda kitu pasipokuwa na chochote.

Mnamo 2006, chama cha Raga cha Kenya (KRU) kilimteua Benjamin Ayimba kuwa mchezaji na kocha wa timu ya kitaifa ya wachezaji saba katika kilichotakiwa kuwa kuzindua upya mfumo kwa lengo la kuimarisha mambo.

Timu hiyo ya wachezaji saba haikuwa ilivyo wakati huu. Kenya ilikuwa bado taifa changa lililokuwa likijaribu kufikia timu ambazo zilikuwa zimeweka mifumo thabiti ya kutambua na kukuza vipawa. Timu kama New Zealand, Australia, Afrika Kusini, Fiji na Ufaransa zilikuwa mbele sana. Kenya ingeweza tu kualikwa kwa mashindano machache ya Raga ya wachezaji saba duniani wakati huo.

Lakini hata enzi hizo, Kenya ilikuwa ikivutia umati. Mashabiki kote duniani walipenda timu hiyo kwa sababu uchezaji wake ulitumia maarifa na kasi, jambo ambalo liliisaidia kupata ushindi mkubwa baadhi ya nyakati.

Alipokuwa akiunda timu yake ya kushiriki Dubai Sevens mnamo 2006, Ayimba alimjumuisha Injera, mchezaji matata wa raga aliyekuwa na kasi sana. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa umaarufu wa Ayimba, Injera na timu ya taifa ya wachezaji saba.

Kenya ilimaliza msimu wa 2005-2006 katika nafasi ya saba, kwa jumla ya alama 13. Timu hiyo ilishuka alama 11 msimu uliofuatia, lakini ikaimarika kwa jumla ya alama hadi 22.

Katika msimu wa 2007-2008 ulimwengu ulianza kufuatilia Kenya na baadhi ya wachezaji wake hodari kama Injera.

Aina ya raga ya Ayimba ilifanya

Nation Media Group "Digital Copy"

# kurunzi ya kenya

Kenya kutoka kuwa ya kufurahisha umati hadi kuwa washindani wa kila mara wa nafasi ya robo fainali katika kila shindano. Timu ilimaliza katika nafasi ya saba ikiwa na alama 38.

Kenya ilikuwa ikicheza raga nzuri, na magoli ya Injera yalikuwa yakiongezeka. Lakini ni msimu wa 2008-2009 ambao Injera aliweka rekodi. Mchezaji huyo winga wa Mwamba RFC alifunga magoli 42. Hakukuwa na ushindani, kwa kuwa mshindani wa karibu alikuwa Rayno Benjamin wa Afrika Kusini akiwa na magoli 28. Injera alipata jumla ya alama 210 msimu huo. Alishindwa na Ben Gollings pekee wa England aliyezoa alama 260.

Injera alikuwa mchezaji wa pekee aliyekuwa katika orodha mbili za magoli na alama. Pia alikuwa mchezaji wa pekee miongoni mwa wafugaji 10 wa magoli yasiyokuwa ya kukamilisha.

Msimu huo hakuna aliyeweza kumsimamisha Injera; alifunga kwa urahisi na hangekosea. Juhudi zake zilikweza Kenya hadi nafasi ya sita kufikia mwisho wa msimu huo ikiwa na alama 64, nafasi yake bora kushikilia wakati huo.

Mnamo Machi 5, 2009, Dubai iliandaa mashindano ya Dunia ya Raga ya Wachezaji Saba. Kenya ilishiriki shindano hilo ikiwa timu ya kupigiwa upatu kufuatia ilivyofanya msimu uliotangulia.

Kwa kuwa haikuwa imefika Kombe la Dunia, presha ilikuwa nyingi, ikizingatiwa matarajio yalikuwa juu. Lilikuwa shindano la ajabu kwa kuwa timu kubwa zilizopigiwa upatu - New Zealand, Afrika Kusini na Fiji- ziliondolewa katika robo fainali. Kenya ilikuwa imepata sifa ya kuangusha miamba, na ilikuwa imewahi kushinda kila timu kubwa katika mashindano ya dunia ya wachezaji saba kila upande, isipokuwa Fiji.

Katika robo fainali ya kombe la dunia mnamo 2009, Kenya ilipata ushindi wa kwanza dhidi ya kisiwa hicho cha bahari ya Pacific kwa magoli 26 kwa 7. Dakika chache katika kipindi cha kwanza, Lavin Asego alichenga walinzi wa Fiji kufunga bao la kwanza na kutangaza nia ya Kenya.

Injera, Kayange na Biko Adema wote walifunga katika kipindi cha pili na Kenya ikaingia nusu fainali dhidi ya Argentina. Argentina ilishinda Kenya 12- 0 katika semi fainali kabla ya kubwagwa na Wales katika fainali.




| | |
|---|---|
| **Jina:** Collins Injera | |
| **Kuzaliwa:** Okota 18, 1986 | |
| **Klabu:** Mwamba, Ulinzi | |
| **Mechi za kitaifa:** Shujaa (7s) 2006-2022, Simbas (15s) 2011-2022 | |
| **Mkewe:** Chebet Limo | |
| **Watoto:** Watatu | |
| **Ndugu:** Humphrey Kayange, Michael Agevi | |
| **Elimu:** Digrii ya Uanahabari kutoka Chuo Kikuu cha Daystar | |
| **Uraibu:** Gofu | |

Bado ulikuwa msimu bora kwa Kenya na Injera, na aliteuliwa mchezaji Bora Duniani wa Raga ya Sevens wa mwaka msimu wa 2008-2009. Injera pia aliwakilisha Kenya katika mechi za kufuzu kombe la dunia la raga ya wachezaji 15 kila upande 2011 na 2022 ambapo nchi haijakuwa na bahati sana. Miaka hiyo miwili, Kenya ilishindwa katika fainali na Namibia. Aliendelea kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa timu ya wachezaji saba hadi alipostaafu. Aliachwa nje mara kadhaa katika uteuzi wa timu katika miaka michache ya hivi majuzi, lakini kukosekana kwake kulikuwa na athari wazi.

Mnamo Mei 2015, Injera alikuwa Mwafrika wa kwanza kufikisha magoli 200 katika mashindano ya Raga ya Duniani.

Ufanisi huu ulijiri katika ushindi wa magoli 24 kwa 12 dhidi ya Japan katika shindano la London Sevens, kuelekea mwisho wa msimu wa 2014-2015.

Tukio hilo lilijiri na sherehe za aina yake ingawa zilikumbwa na mzozo. Baada ya kutua nchini, mchezaji huyo aliyekuwa na umri wa miaka 29, alichomoa kalamu ya wino mzito kutoka ndani ya soksi zake na kutia saini kamera ya Sh9.2 milioni.

Habari zilisambaa kuwa kalamu ya wino usiofutika ya Injera ilikuwa imeharibu kamera hiyo, lakini hilo limekanushwa na wadau kadhaa, akiwemo gwiji huyo wa Kenya. Wakati huo, Santiago Gomez Cora wa Argentina alikuwa akiongoza kwa ufungaji wa mabao katika mashindano ya dunia ya wachezaji saba akiwa na mabao 230. Mchezaji mwingine aliyekuwa amefunga zaidi ya mabao 200 alikuwa Ben Gollings wa England.

Katika msimu wa 2015-2016 Injera alifunga mabao 32 na kufanya yake kuwa 235 na kumwezesha kushinda Gollings na Cora.

Alishinda goli muhimu sana la 231 dhidi ya Ufaransa katika mechi ya mwisho ya makundi katika shindano la London Sevens. Winga huyo mwenye kasi alikimbia katika eneo la kuketi mashabiki, akatoa jezi yake na kuwapa wazazi wake wakikumbatiana kwa furaha na kuzidiwa na hisia.

Kama kulikuwa shaka awali, sasa ilikuwa wazi alikuwa hodari wa mchezo huo. Mawili ya magoli hayo yalijiri wakati bora zaidi - katika fainali za Singapore Sevens ambapo Kenya ilishinda Fiji 30-7 kupata ushindi wake wa kwanza kabisa.

Ayimba, ambaye muhula wake wa kwanza akiwa kocha ulimfungulia milango Injera, alikuwa amerudi msimu ukiwa kileleni. Kurudi kwake kulimfanya Injera kupata tuzo muhimu zaidi katika kazi yake - wa kwanza katika orodha ya wafungaji mabao na tuzo ya mfungaji bora wa shindano. Ulikuwa msimu wa ushindi kwa Injera, kwa Kenya na kwa raga. Winga huyo hakuwa mtu wa kukaa chini baada ya kuteleza. Mwaka wa 2011, aliondolewa kutoka timu ya taifa kufuatia mzozo kuhusu malipo.

Aliyekuwa kocha wakati huo Mike Friday aliagiza wachezaji wapumzike baada ya mikumbo ya Wellington na Las Vegas. Lakini klabu ya Injera, Mwamba, ilikuwa imeingia nusu fainali za Kenya Cup na ilimtaka acheze. Injera hakucheza, kwa hivyo, klabu ilimsimamisha kwa wiki nane na kumuagiza asishiriki mazoezi ya timu ya Kenya Sevens.

Injera hakufanya mazoezi na timu ya taifa alivyoagizwa, kwa hivyo kandarasi yake ilifutwa.

Friday alimwambia Injera kuwa alifahamu alichopaswa kufanya kurudishiwa kandarasi yake. Ingawa masharti hayo hayajawahi kutolewa hadharani, Injera alirudi katika timu kumaanisha alifanya alichotakiwa kufanya.

Injera amestaafu. Na safari yake imemalizika kwa magoli 279 katika mashindano ya dunia ya wachezaji saba, na heshima ya wadau wote wa raga. Dan Norton wa England amefaulu kufunga mabao 358, na kufanya Injera wa pili katika orodha ya wanaoongoza kwa mabao. Injera amecheza mashindano manne ya Kombe la Dunia ya Wachezaji Saba, ameshiriki mechi 424 katika mashindano 83 - nyingi zaidi kuchezwa na Mkenya - na kushiriki Olimpiki mara mbili.

Ameshinda Safari Sevens mara kadhaa, akashinda mashindano ya humu nchini ya wachezaji saba akiwa na Mwamba na ameshiriki michezo ya Madola akichezea Kenya. Alikuwa mchezaji bora wa mwaka wa 2009 (Soya). Aliyekuwa Rais Mwai Kibaki alimtuza Injera Order of the Grand Warrior mnamo 2009.

Tofauti na yaliyotokea kuhusu kamera ya thamani ya Sh9.2 milioni, saini ya Injera katika chandarua cha raga ya wachezaji saba haitafutika katika vitabu vya historia.

***bwasuna@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Microsoft sasa kutia mabilioni katika OpenAI




Microsoft imetangaza uwekezaji wa miaka mingi wa mabilioni ya dola katika akili ya kisasa (AI) huku ikipanua ushirikiano wake na OpenAI.

OpenAI ndiye alitengeneza chombo maarufu cha kutoa picha ya Dall-E na chatbot ChatGPT. Mnamo 2019 Microsoft iliwekeza Sh123 bilioni kwa kampuni hiyo iliyoanzishwa na Elon Musk na mwekezaji wa teknolojia Sam Altman.

Watengenezaji wa Windows na Xbox wanapanga kufuta kazi watu kufikia 10,000 lakini walisema bado wataajiri katika maeneo muhimu ya kimkakati. Akitangaza hayo kupitia barua kwa wafanyakazi wiki iliyopita, afisa mkuu mtendaji Satya Nadella alisema "Wimbi kuu linalofuata la kompyuta linatokana na maendeleo katika AI."

Kampuni hiyo ilisema inaamini AI itakuwa na "athari kwa ukubwa wa kompyuta ya kibinafsi, mtandao, vifaa vya rununu na wingu". ChatGPT inaweza kutoa majibu ya kibinadamu kwa maswali.

Uvumi kuhusu uwezekano wa matumizi mabaya ya teknolojia, kutoka kusaidia wanafunzi danganya katika mitihani hadi kuandika program mbaya, umeandamana na mapendekezo kuwa ina uwezo wa kuleta mapinduzi katika tasnia nyingi, ikiwepo utafutaji.

Microsoft inamiliki injini ya utafutaji ya Bing, na huku ikiwa nyuma ya Google kwa umaarufu, wengine wanapendekeza kuwa ChatGPT inaleta tishio kwa kiongozi wa sekta hiyo. Gazeti la New York Times liliripoti kuwa hatua hiyo imefanya Google kutangaza "msimbo mwekundu" ikihofia inaweza kunyakua soko la kampuni hiyo ya thamani ya Sh 18.3 trilioni.

Awali, Google ilisita kutoa baadhi ya mifumo ya AI kwa matumizi ya umma.

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# DARUBINI YAWINDA ASILI YA KIKEMIKALI YA MAISHA



Vioo vya darubini ya James Webb Space vikifanyiwa majaribio katika kituo cha shirika la Nasa cha Marshall Space Flight Centre mjini Huntsville, Alabama.

● LONDON

Darubini mpya ya anga ya juu James Webb imejitosa imeingia eneo la baridi kali. Imekuwa ikichunguza baadhi ya maeneo yenye giza na baridi zaidi angani kwa vidokezo kuhusu kemia inayotengeneza sayari, na pengine hata maisha.

Picha hii mpya iliyotolewa inaonyesha sehemu ya wingu la molekuli ya Chameleon I, karibu miaka 630 ya mwanga kutoka duniani.

Ni hapa, kwa joto la chini hadi karibu -260C, ambapo Webb inagundua vipande vya barafu ambavyo hazikuonekana awali. Hatimaye, mawingu hayo yataanguka na kuunda nyota na sayari karibu nayo. Na kemia inayochunguzwa na Webb itajumuishwa. Unaweza kuona hili juu-kushoto ya picha.

Sehemu rangi ya chungwa ya "kipima muda" ni protostar - nyota katika hali ya malezi, ikivuta kwake nyenzo kutoka kwa wingu.

Nyota za rangi ya chungwa zilizo chini zimekomaa zaidi na zinang'aa vya kutosha hivi kwamba zinatia miiba sita ambayo sasa imefahamika katika picha za Webb na ni kazi za sanaa za muundo wa kioo wa darubini iliyogawanywa. Lakini ili kugundua barafu, Webb inapuuza nyota hizi zote kando na kuangalia nyota nyuma ya Chameleon I ya rangi samwati. Mwanga kutoka kwa vitu hivi unapomulika kupitia wingu, baadhi yake humezwa na barafu ili kubadilisha muundo wake.

"Ni kama mfano wa kivuli" akaeleza Dk Melissa McClure kutoka Chuo Kikuu cha Leiden, Uholanzi. "Una aina fulani ya umbo linalotengeneza kivuli. Barafu hufyonza kwa urefu fulani mawimbi ya mwanga na unaongeza hizo zote kwenye wigo ili kuona ni aina zipi za kemikali ulizo nazo," akaambia BBC News.

Hii ni kazi inayofanywa hasa kwenye Webb na spektrometa zake za karibu kwa kiwango fulani na kamera yake ya ambayo ilitoa picha nzuri juu ya ukurasa.

Mbali na barafu rahisi kama vile maji, kaboni dioksidi, kaboni monoksidi, amonia, na methane, Webb huona misombo mingine kadhaa, ikiwemo carbonyl sulphide na methanol ya barafu ya kikaboni (iliyo na kaboni). Na kuna vidokezo, pia, vya aina za kemikali zilizo na atomi nyingi za kaboni kama vile asetoni, ethanol, na asetaldehyde.

Ni rahisi zaidi kwa wataalamu wa anga kuona shabaha hizi angani zikiwa gesi. Webb inavunja msingi mpya kwa kuziona katika hali thabiti, kama barafu. Itasaidia wanasayansi wanapojaribu kuelewa ilikotoka kemia ya maisha na jinsi ilivyojenga ustaarabu unaoonyesha sasa kwenye sayari yetu.

"Ingawa tuligundua barafu zaidi kuliko ilivyowahi kuripotiwa, kiasi cha 'chembe nyepesi' (kaboni, hidrojeni, oksijeni, nitrojeni, na salfa) zilizo ndani yake bado ni kidogo kuliko tunavyotarajia," akaeleza Dk Helen Fraser, wa Chuo Kikuu cha Open, Uingereza.

"Kwa wanaastronomia hiyo inasisimua, kwa sababu inamaanisha kuna kitu ambacho bado hatuelewi kikamilifu kuhusu kemia kati ya nyota - na ambacho kinatupa changamoto sio tu kuendelea kutazama, lakini pia kufanya majaribio katika maabara."

Karibu na nyota mpya inayojitengeneza, vumbi lenye barafu kama zile za Chameleon ingeyeyuka mara nyingi, lakini zaidi zingeweza kuishi na kukusanyika pamoja kutengeneza kometi.

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

# kurunzi ya afrika

■ MBINU YA 'KUCHELEWESHA KESI KWA VYOYOTE' MEFIKIA KIKOMO

# CHUMA CHA ZUMA MOTONI



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa (kulia), akisalimiana na mtangulizi wake, Jacob Zuma, wakati wa karamu ya kumuaga Zuma katika Ikulu ya Cape Town mnamo Februari 20, 2018. PICHA I AFP

## Bila 'mabadiliko' katika mwelekeo wake wa sasa, aliyekuwa rais na mfungwa mara mbili anaonekana kuwa tayari kwa kipindi kingine cha kuvaa 'suti rangi ya chungwa'

● NA CHRIS ERASMUS

Kama mwaka wa 2022 uliisha vibaya kwa Jacob Zuma - na ilikuwa hivyo - matarajio ya rais huyo wa zamani wa Afrika Kusini mwaka wa 2023 na kwenda mbele ni mabaya zaidi.'Shida kamili' za Zuma zinaanza Jumatatu, anapotarajiwa kurudi kortini kwa mashtaka ya ufisadi.

Wiki iliyopita, kikao kamili cha Mahakama Kuu kilitoa uamuzi uliomfaa Rais Cyril Ramaphosa kuwa Zuma alikuwa akitumia vibaya taratibu za kisheria kwa kumtaja Ramaphosa katika juhudi zake za kuwashtaki kibinafsi mwendesha mashtaka wa serikali katika kesi ya ufisadi iliyodumu kwa muda mrefu ya rais huyo wa zamani na mwanahabari ambaye amekuwa akiripoti kuhusu safari nyingi za Zuma kwenda mahakamani. Uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu iwapo Zuma anaweza kumtaja Ramaphosa kwa kutovunja sheria, ulitolewa kabla tu ya kesi ambapo Ramaphosa alikuwa ameitwa kortini kuhusu mashtaka ya kibinafsi ya Zuma.

Malalamishi ya Zuma yalikuwa kwamba Ramaphosa hakumuondoa au kumchukulia hatua Wakili wa Serikali Billy Downer, mwendesha mashtaka ambaye Zuma anataka aondolewe kwa madai ya 'upendeleo'.

Mawakili wa Ramaphosa walikuwa wameeleza jopo la majaji watatu kuwa ombi la Zuma lingekuwa kinyume cha katiba, kama lingeshughulikiwa, na kuwa Ramaphosa hakufanya uhalifu kwa kutochukua hatua yoyote. Maoni ya kisheria katika kesi hii ya aina ya kipekee ambayo haijawahi kuonekana ambapo Zuma amehusisha Downer, mwandishi wa habari Karyn Maughan na Ramaphosa, ni kwamba ni "mkakati wake wa kujitetea", akitumia kila mbinu ya kisheria ya kuchelewesha

...Endelea Uk 26

# Zuma taabani kesi ya ufisadi ikiendelea

Kutoka Uk 25

kesi na huku akitafuta zingine mpya.

Ukweli ni kuwa, 'sarakasi' ya mashtaka ya kibinafsi ya Zuma ikimalizika tu, na bila matumaini ya kufaulu kwa msingi wa ukweli unaojulikana, ni lazima Zuma Jumatatu atakabiliwa na kuanza kwa kesi yake kuhusu mkataba wa silaha wa miaka ya 1990 ambapo inadaiwa alipokea hongo.

Aliyekuwa "mshauri wa fedha" wa Zuma alihukumiwa kifungo cha miaka 15 jela - lakini alitumikia kifungo kifupi tu, na kuachiliwa katika kinachoonekana kuwa uongo wa "sababu za kimatibabu" - kwa mashtaka 783 ya ulaghai, ulanguzi wa pesa na ufisadi, sawa na yanayomkabili Zuma.

Juhudi za kutaka mwendesha mashtaka Downer, ambaye alifaulu kumshtaki mshauri wa kifedha wa Zuma, aondolewe katika kesi hiyo zilichelesha kesi hiyo 2022 na mawakili wa Zuma wanaonekana kutaka kuchelewesha mambo zaidi, wakipata nafasi hiyo.

Zuma pia amejaribu kumtaka jaji anayesikiliza kesi yake ya ufisadi ajiondoe, pia kwa madai ya kupendelea, wito ambao jaji huyo amekataa na kuungwa mkono na majopo ya juu. Isipokuwa mashtaka ya kibinafsi anayotaka kuanzisha kwa misingi dhaifu, Zuma sasa anakabiliwa na sheria bila namna nyingine ya kuchelewesha kuanza kutolewa kwa ushahidi, na huku kukiwa na mashahidi kadhaa na stakadhi kukaguliwa na mahakama.

Isipokuwa tu mawakili wa Zuma "wawe na jinsi ya kiajabu ya kumuondolea lawama", akasema mchanganuzi mkuu wa masuala ya sheria, hakuna sababu ya kuamini kuwa mahakama katika kesi yake ya ufisadi haitafikia uamuzi sawa, kwa ushahidi sawa.

Kwa upande wa kisiasa, mambo pia yanamwendea vibaya rais huyo wa zamani. Zuma na wengi wa wanaomuunga mkono, likiwemo kundi dogo la "simba wachanga" la vijana chama tawala cha African National Congress (ANC) katika jimbo analotoka Zuma la KwaZulu-Natal, walishindwa vibaya katika kongamano la uchaguzi wa kila miaka mitano wa ANC, uliomalizika mwisho wa Desemba.

Chama cha ANC katika eneo la Zuma, ambalo ndilo kubwa zaidi kwa idadi ya watu, kimekuwa kikimuunga mkono na kilituma karibu robo ya wajumbe wa kupiga kura kwa kongamano hilo lakini kilipata sehemu ndogo sana ya viti 87 vya baraza kuu la kitaifa la chama tawala, na hakikupata nafasi saba za juu.

Hilo, kwa lugha ya kisiasa, ni pigo kubwa, hasa kwa sababu Zuma na washirika wake wa karibu walipanga kongamano hilo kama "mtego" dhidi ya Rais Ramaphosa, kwa nia ya kumuondoa katika uongozi wa chama na serikali. Ulikuwa mpango wa 'kumzuia' Ramaphosa kugombea muhula wake wa pili. Lakini Ramaphosa aliepuka njama hiyo iliyokitwa kwa misingi ya 'kashfa ya shamba la wanyama la Phala Phala' ambapo dola 580,000 (Sh71.3 milioni) ziliibwa, na akashinda kwa urahisi huku umaarufu wake ukiongezeka katika ngazi za juu za chama. Katika mpango wa kumuondoa mamlakani Ramaphosa, Zuma na wenzake walitarajia kufikia 'mabadiliko' katika jaribio la karibu miongo miwili la kukwepa kujibu mashtaka ya ufisadi.




Wafuasi wa Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa wakisherehekea alipochaguliwa tena kuongoza chama cha African National Congress wakati wa Kongamano la Kitaifa la 55 la ANC katika Ukumbi wa Kitaifa wa Burudani (NASREC jijini Johannesburg mnamo Decemba 19, 2022.
PICHA I AFP

Bila 'mabadiliko' katika mwelekeo wa sasa wa Zuma, aliyekuwa rais na mfungwa mara mbili - wakati wa ubaguzi wa rangi alipotumikia kifungo cha miaka 10 kwa kupinga ubaguzi wa rangi, na hivi majuzi miezi miwili ya kifungo cha miezi 15 kwa kupuuza mahakama – anaelekea kuvaa tena 'suti rangi ya chungwa', ambayo ndiyo sare ya wafungwa.

Hata hivyo, huenda ushahidi wa kesi ya Zuma kuhusu hongo katika mkataba wa kununua silaha ukacheleweshwa tena jaji anayesikiliza kesi hiyo akiamua kujiondoa, baada ya kukataa ombo hilo hapo awali. Jaji wa Mahakama Kuu ya Pietermaritzburg, Piet Koen, ambaye 'uadilifu' wake umepongezwa na kushambuliwa na mawakili wa Zuma, atashughulikia pingamizi za mwisho za Zuma kabla ya ushahidi kuanza kutolewa.

Mara kadhaa mawakili wa Zuma walipotumia mbinu za kujitetea kwa lengo la kuchelewesha kesi, Jaji Koen alionekana kukasirika lakini alivumilia ili kuepuka dalili zozote za kumuonea Zuma.

Malalamishi kutoka kwa mawakili wa Zuma kuhusu hatua za mwanzo za kesi hiyo yalisababisha kinachojulikana kama "hatua ya kukata tamaa" ya mashtaka ya kibinafsi ya Zuma dhidi ya mwendesha mashtaka Downer katika hatua ya mwisho, lakini karibu kushindwa, kujaribu kumuondoa Downer katika kwa kesi. Kuondolewa au kujiondoa kwa jaji au mwendesha mashtaka mkuu kunaweza kuchelewesha zaidi kesi hiyo, hali ambayo mawakili wa Zuma wamekuwa wakiitafuta na bado wanaitafuta.

Madai dhidi ya Downer ambayo hayajathibitishwa, na ambayo si muhimu, 'upendeleo' ndiyo yalimfanya Zuma ajaribu kwenda hadi Mahakama ya Kikatiba, ingawa hakufaulu, kutaka Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali aondolewe, kwa sababu 'upendeleo' huo unamvua Downer "cheo cha kisheria kufanya kazi".

Huu ni msimamo wa kisheria usiokubalika ambao haujawahi kujaribiwa awali, na uliotupiliwa mbali kabisa majuzi na Mahakama ya Kikatiba kuwa batili. Sababu ya chuki ya Zuma dhidi ya Downer ni mafanikio ya mwendesha mashtaka huyo kumfungulia mashtaka rafiki wa karibu wa Zuma na mshauri wake, Schabir Shaik, katika suala lhilo hilo la hongo katika mkataba wa kununua silaha, mashtaka ambayo pia yanamkabili Zuma.

Kufikia mwanzo wa 2023, mbinu ya 'kuchelewesha kwa vyoyote' imeondolewa katika mfumo wa sheria wa Afrika Kusini.

Lakini kila rufaa inayoendelea ni msingi wa mawakili wake kudai, tena, kuwa kuna mambo muhimu yanayozingatiwa na mahakama zingine, nkwa hiyo kesi haiwezi kuendelea. Hata hivyo, siku moja hivi karibuni, rufaa na mbinu za kuchelewesha zote zitafikia kikomo, kisha Zuma ataachwa peupe kukabili sheria.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "Digital Copy"

## kurunzi ya dunia

■ KATIKA LYMAN, WAKAZI 13,000 WANAISHI KATIKA HALI YA BARIDI KALI

# MAISHA YA HUKO NI JEHANAMU



Wanajeshi wa Ukraine wakifyatua makombora ya ardhini aina ya MLRS kuelekea maeneo ya Urusi katika mstari wa mbele wa vita eneo la Donbas, mashariki mwa Ukraine mnamo Juni 7, 2022.

### Licha ya vita vikali vinavyoendelea eneo la Donbas, raia wameanza kurudi katika miji ya Ukraine iliyokombolewa karibu na eneo la vita

• KYIV

Ndege mbili za kivita za Ukraine zinavuma angani, kwa karibu, tunapotoka ndani ya msitu uliofunikwa na ukungu na kuendesha gari letu hadi mji wa Lyman, ulioko kwenye makutano ya reli, eneo la Donbas, mashariki mwa Ukraine.

Ni karibu miezi minne tangu wanajeshi wa Urusi walipolazimika kuondoka hapa, wakasukumwa umbali wa kilomita 25 eneo la mashariki. Lakini milio ya mizinga, karibu na eneo la vita, bado inasikika kila dakika. Mji huu ambao sehemu yake kubwa imeharibiwa, bado si salama kutokana na makombora yanayorushwa na wanajeshi wa Urusi.

"Naishi orofa ya saba. Roketi hiyo iligonga orofa ya tano, alfajiri, mwendo wa saa kumi na moja. Lakini niko salama," akasema Alecander Rogovitz, 73, mfanyabiashara mstaafu. Ndiye mkazi pekee aliyebakia katika jengo hilo la makao pembeni mwa mji.

Anainama kuwapa paka wanane chakula kilichokaushwa, saba kati yao ni waliachwa na majirani zake na sasa anawatunza.

Watu walioamua kubaki katika ukungu na vifusi hapa wanaonekana wenye bidii na moyo wa umoja. Katika kibanda kilicho karibu, fundi wa reli Valeri Dmitrenko, 45, anaendelea kupasua kuni za kupasha joto sehemu ya chini ya jengo ambako yeye na majirani wamekuwa wakikaa kwa miezi tisa iliyopita. Mji wa Lyman bado hauna maji ya mfereji na mitambo ya kutoa joto na kuna baridi kali nyakati za mchana.

"Tufanye nini?" Valeri anauliza akitikisa mabega huku akipapasa kichwa cha mbwa koko ambaye yeye na mkewe, Ira, wameamua kumlea na kumpa jina, Princess Diana. Asipokuwa akipasua kuni, Valeri husaidia majirani kukarabati milango na madirika katika jengo lao lililoharibiwa vibaya.

Endelea Uk 28

Nation Media Group "Digital Copy"

# Maisha ya hofu: 'Jehanamu' nchini Ukraine

Kutoka Uk 27

Ira anapita, haraka, akibabe ndoo za maji aliyoteka kutoka kwa kisima kilicho karibu.

"Bado ni vigumu kwangu kukaa nje kwa muda mrefu," anasema Ira, 45, kabla ya kuelekea chini, kwa ngazi, hadi chumba chake chini ya jengo lililo kando ya barabara ya 6 Railways Street.

Licha ya vita vikali vinavyoendelea Donbas, raia wameanza kurudi katika miji ya Ukraine iliyokombolewa karibu na eneo la vita. Hii ni kinyume cha ushauri kutoka kwa maafisa wa utawala eneo hilo. Katika mji wa Lyman, ulioharabiwa na wanajeshi wa Urusi mwaka jana, wakazi 13,000 wanaishi katika mazingira magumu ya msimu wa baridi.

Wanajeshi wa Urusi walipokaribia Lyman Juni mwaka jana, raia 41,000 walitoroka na kuacha nyuma watu 10,000, wengi wakiwa wakongwe, maskini au watu kama Ira na Valeri ambao jamaa zao ni wagonjwa kwa hivyo wakakataa kuondoka. Katika miezi minne iliyofuata, karibu watu 60 walisongamana katika nyumba hiyo katika Railway Street. "Nyakati zingine ilikuwa vigumu. Watu ni tofauti. Wengine waligeuka wakorofi - hatujazoea kuishi pamoja jinsi hii," akasema Ira.

Kuongezea masaibu yao, karibu thuluthi moja ya walioamua kuishi katika nyumba hiyo wanaunga mkono Urusi, wakitumai kuwa Ukraine itashindwa katika vita hivyo. "Ndio kuna watu waliounga mkono Urusi. Lakini waliondoka Ukraine ilipoanza kukomboa eneo hilo. Wavamizi wa Urusi walipoondoka, walienda nao, pamoja na watoto wao. Labda walihofia maisha yao hapa," anaongeza.

Mnamo Oktoba 3, mji wa Lyman ulikombolewa na wanajeshi wa Ukraine na baadaye meya wa mji huo Alexander Zhuravlyov akarudi na kugundua kati ya asilimia 80 na asilimia 90 ya majengo yalimeharibiwa. Njia za reli zinazopitia katikati mwa mji bado zimejaa nyaya za stima zilizokatwa na njia zilizofungwa.

Katika miezi ya hivi majuzi, meya huyo na maafisa wake walifaulu kurudisha stima katika sehemu nyingi za mji na vijiji vinavyouzunguka. Malipo ya pensheni sasa yanatolewa kwa wakati na baadhi ya maduka yamefunguliwa tena.

Serikali na makundi ya kutoa misaada ya kibinadamu yameleta majiko ya kuni na kusambaza magogo. Kila siku kundi moja la kutoa misaada huleta vyakula vilivyopikwa na kupakiwa na kuwasambazia wakazi bila malipo. Kuna watoto karibu 700 wanaoishi mjini Lyman na meya anakadiria kuwa wakazi wengine 3,000 wamerudi tangu mji huo ulipokombolewa. Lakini anawashauri wengine wasirudi.

"Kwa sasa hatungependa watu warudi hapa. Wako salama katika miji na sehemu waliko. Hakuna sehemu salama za kuishi hapa sasa. Watu watakubaliwa maeneo mengine na watapewa malazi na chakula," akasema akiendesha gari lake kuelekea eneo ambako ukuta wa jengo la orofa tisa uliharibiwa na makombora wiki mbili zilizopita.



Mwanamke mkongwe akilalamika baada ya nyumba yake kulipuliwa kwa kombora wakati wa makabiliano ya makombora kati ya wanajeshi wa Ukraine na Urusi mjini Lysychansk, eneo la Donbas, mashariki mwa Ukraine, mnamo 11, 2022. PICHA I AFP

Meya anasema polisi wa eneo hilo bado wanapambana na wakazi wachache wa Lyman wanaoshukiwa kushirikiana na wavamizi wa Urusi. Lakini anaamini matukio ya mwaka uliopita yamewafanya wakazi wengi waliounga mkono Urusi kubadili misimamo yao.



Mwanamke akilia nje ya nyumba yake iliyoharibiwa baada ya shambulio mjini Slovyansk, eneo la Donbas, mashariki mwa Ukraine mnamo Mei 31, 2022. PICHA I AFP

"Nafikiri watu hao sasa wanaelewa kuwa walikosea. Walipotoshwa na vyombo vya habari - wakitazama propaganda za Urusi kwa televisheni kila usiku na kufikiria ilikuwa kweli. Walikuwa wachache na wamebadili misimamo yao. Wamegundua hali ya Urusi siyo waliyokuwa wameambiwa watarajie," akasema Zhuravlyov.

Mwanamke wa miaka 62 kwa jina Valentina, akipiga foleni kupewa chakula katika hospitali moja, anaonekana kubadili msimamo anapoulizwa kuhusu hali ya usalama mjini Lyman tangu ulipokombolewa. Katika miezi ya hivi majuzi, raia wanaounga mkono Urusi walionyesha miegemeo yao walipodai pande zote mbili zilisababisha uharibifu wa miji. Walisema haiwezekani kulaumu upande mmoja.

"Mashambulio hayajasitishwa. Mabomu bado yanagonga mji huo. Hatujui anayeyarusha," anasema Valentina. Lakini ghafla anabadilisha msimamo wake. "Nadhani lazima ni Warusi. Ndio, bila shaka ni wao," anasema huku akiongeza: "Sisi ni raia wa Ukraine. Huu ni mji wa Ukraine. Maduka yamefunguliwa. Pensheni zetu zinakuja kwa wakati. Serikali haijatusahau."

*- BBC*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "Digital Copy"

kurunzi ya dunia

■ INALENGA KUVUTIA WAKRISTO I MILIONI 2030

# UKARABATI WA ENEO ALIKOBATIZWA YESU

**Mwezi huu ndio msimu wa wageni wengi huku mahujaji wa makanisa ya Orthodox ya Magharibi- na kisha Mashariki- yakisherehekea Epiphania**



Mahujaji wa Kanisa Katoliki wahudhuria ibada nje ya Kanisa la Mtakatifu Yohana Mbatizaji, karibu na eneo la ubatizo la Al-Maghtas, mnamo Januari 13. Wakristo wanaamini Yesu alibatizwa na mtakatifu huyo katika eneo hilo, ndani ya Mto Jordan, karibu kilomita 60 kusini-magharibi mwa mji mkuu wa Jordan, Amman. Maelfu ya Wakatoliki hufika kwa ibada hiyo maalumu kwenye kingo za Mto Jordan kila mwaka. PICHA I AFP

● LONDON

Leo Mto Jordan hauwezi kulinganishwa na uliotajwa katika Bibilia, lakini wageni wapatao 200,000 bado hufurika katika eneo la kitamaduni la ubatizo la Kikristo katika Jordan kila mwaka.

Ninatazama makundi kutoka Amerika na Ulaya yakibadilishana zamu kujitosa kwa uangalifu katika upana wa maji yenye matope na kujipiga picha kwenye kingo za mto huo. "Ukiwa eneo hili, lazima ufike hapa. Ni sehemu ya historia," anasema Oliver, ambaye ni Mfaransa. Mark kutoka Maryland anasema alikuja "kwa sababu ya kiroho, aweze kufuata nyayo za Yesu."

Mwezi huu ndio msimu wa wageni wengi huku mahujaji wa makanisa ya Orthodox ya Magharibi- na kisha Mashariki- yakisherehekea Epiphania. Likizo hiyo ni ya kuadhimisha ziara ya Wanaume Watu Wenye Hekima au Magi, kumuona mtoto Yesu, na kubatizwa kwake na nabii Yohana. Hivi majuzi, Jordan ilitangaza mpango mkubwa wa dola 100 milioni unaolenga kuvutia Wakristo milioni moja eneo la Al-Maghtas mwaka wa 2030, kuadhimisha kinachoaminiwa kuwa mwaka wa 2000 tangu kubatizwa kwa Yesu.

"Inakuwa furaha kupata wageni wetu, mahujaji wetu, wakishuhudia kile Yohana na Yesu walifanya," anasema Rustom Mkhjian, mkurugenzi mkuu wa eneo la ubatizo la Jordan. "Ninaiita 'injili ya tano', kwa kuwa unaona kwa macho unachosoma katika injili zote nne. Unahisi kuwa katikati ya historia ya dini na imani."

Eneo la ubatizo, ambalo pia linajulikana kama Bethania Ng'ambo ya Jordan, ni eneo la ukumbusho Ulimwenguni la Unesco, ambako mabaki ya makanisa ya Kirumi na Bizantinia, nyumba ya utawa na vidimbwi vya ubatizo vimehifadhiwa katika mwitu karibu na sehemu ya chini ya ardhi. Vilivumbuliwa mnamo 1995 baada ya mkataba wa amani na Israeli.

Awali, pande mbili za mto huo zilikuwa eneo la vita lililofungwa tangu vita vya Mashariki ya Kati mnamo 1967, ambavyo Israeli iliteka Ukanda wa Magharibi kutoka Jordan na kuutwaa. "Kuvumbuliwa upya kwa eneo hilo ni matunda ya amani," Bw Mkhjian ananiambia. "Hebu fikiria, viwanja vikubwa vya vilipuzi viliondolewa vilipuzi vyote. Ninaongea kuhusu maelfu ya vilipuzi vilivyoondolewa. Si ni heri kuwa na mamilioni ya mahujaji badala ya vilipuzi?"

Ingawa raia wa Jordan hushindania watalii na upande wa mto unaodhibitiwa na Israeli, katika miongo miwili iliyopita, papa watatu wa Katoliki, papa wawili kutoka kanisa la Coptic na viongozi wa makanisa kutoka kote ulimwenguni wametembelea al-Maghtas. Watu matajiri na maarufu huleta watoto wao kubatizwa hapa, na kasri ya kifalme ya Jordan imepeleka maji takatifu kwa sherehe za kupatia majina watoto wa kifalme wa Uingereza. Kwa mualiko wa maafisa wa Jordan, madhehebu tofauti ya Kikristo yamejenga makanisa mapya hapa, na mengine mengi yamepangwa kujengwa. Ni eneo nadra sana kuonekana Mashariki ya Kati.

"Inafurahisha moyo," mtalii kutoka Amerika, Sharon, ananiambia, akisifu mpango wa familia ya kifalme ya Jordan. "Tunajifunza ni vitu gani tuliyonavyo yanavyofanana vyao, na kwamba serikali ya Jordan inaanzisha yote haya kupatia kila dhehebu haki ya kutumia ardhi iliyo hapa."

Mpango mkuu wa eneo jipya la ubatizo la ekari 340, karibu na eneo la Unesco, ulizinduliwa mwezi uliopita na Mfalme Abdullah. Samir Murad, anayesimamia wakfu usio wa kupata faida ulioanzishwa na serikali ya Jordan kusimamia mradi huo, anasisitiza kuwa uadilifu wa eneo hilo ni lazima udumishwe.

"Utakuwa ujinga na upumbavu kujaribu kuunda kituo cha kitalii kwa msingi wa biashara na masuala yanayofanana na madhari ya bustani katika eneo takatifu kama hili," akasema. "Tukumbuke kuwa hili ndilo jiji la tatu kwa utakatifu katika Ukristo. Hili ndilo eneo ambalo Yesu alipata wito wake na hivyo basi itakuwa makosa sana kulichafua au kulikiuka kwa njia yoyote." Mipango ya maendeleo hayo mapya inajumuisha kinachoitwa nyumba za kulala zinazofanana na mahema yanayotumiwa na watalii na mikahawa, kuuza chakula kinachokuzwa eneo hilo. Nyaya za Intaneti na Stima zitafichwa chini ya ardhi.

Sehemu kubwa ya eneo hilo itatengwa kwa kilimo na hifadhi ya ndege kulinda mazingira asili. Wanatafuta usaidizi kutoka Bustani ya Kifalme eneo la Kew Uingereza kupata baadhi ya mimea iliyo katika bibilia.

***— BBC***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

TANZIA

■ WENZAKE WALIMTAJA KUWA ALIYETUMIA KIFUA ALIPOTAKA MAMBO YAFANYWE

# MSOMI MPYA MBINGUNI

**Jumba la University Tower, katika Chuo Kikuu Cha Nairobi, daima litabakia ukumbusho kwa wengi waliosoma, kufanya kazi na kupitia humo kama ushahidi wa maono ya Magoha kwa taasisi hiyo**



Aliyekuwa Waziri wa Elimu George Magoha aliaga dunia Januari 24. Kimo chake, sauti na macho yalitosha kuzima maoni tofauti. PICHA I MAKTABA

• NA TOM ODHIAMBO

Mara kwa mara, Profesa George Albert Omore Magoha alionekana hadharani kama mtu asiyetabasamu asilani, mwenye sura ngumu kiasi cha kutojali vitu kama salamu, utani au hata kicheko. Lakini huyu ni mtu ambaye angeangua kicheko cha ajabu wakati uliporuhusu jinsi tu ambavyo angevaa sura ya kazi wakati alipotarajiwa kutulia. Risala nyingi za rambirambi katika vyombo vya habari zimemsifia kama mtu aliyependa mambo kwenda alivyotaka, ambaye angetumia kifua kutimiza malengo, kama mtu mchapa kazi ambaye hakuwa na muda wa kupoteza. Hasa, Magoha mara nyingi alionekana kuwa na kazi nyingi ya kufanya kwa muda mfupi.

Matukio mawili niliyoshuhudia yanaelezea tabia ya kutatanisha ya Magoha. Nakumbuka kisa kimoja kinachoelezea ni kwa nini anatajwa kuwa mchapa kazi aliyefanya juu chini kutimiza malengo yake.

Mnamo Agosti 3, 2019, kuna hafla ya kuzindua kitabu iliyopangwa kufanywa Gem, Yala, Kaunti ya Siaya. Profesa Bethwel Ogot alikuwa ameandaa karamu nyumbani kwake kuzindua kitabu chake kwa jina History of Kisumu: 1901-2001. Watu walikuwa wamekusanyika nyumbani humo kuanzia asubuhi mapema. Wenyeji wa Yala, wageni kutoka Uganda na sehemu nyingine uduniani wanafunzi na wafanyakazi wenza wa zamani wa Ogot, wanahabari, miongoni mwa wengine walimsubiri mgeni wa heshima.

Wakati wa chakula ulipofika, chakula kilipakuliwa. Wageni walionekana kuingiwa na hofu – je, 'mkubwa' aliyetarajiwa kuzindua rasmi kitabu hicho angefika au la? Walipokuwa wakinywa soda kuzima joto kali la siku hiyo, gari kubwa la serikali lilifika ghafla. Magoha alikuwa amefika. Alihudhuria fulani ya umma asubuhi hiyo. Alielekezwa kwa kiti chake. Akapakuliwa chakula, alichokula mbele ya umati. Aliteremsha kwa glasi ya maji kisha akawa tayari kuzindua kitabu. Alisimama na kuzungumza kuhusu kitabu hicho na umuhimu wa maarifa katika jamii kwa muda ambao haukuzidi dakika 20.

Ilitarajiwa kuwa mwana wa eneo hilo, katika kijiji chake, kuzungumza siasa, kuzungumza kuhusu ndoto za watu wake na kile serikali ingewafanyia. Magoha wakati huo alikuwa Waziri wa Elimu. Alikuwa mtu mkubwa katika serikali. Kwani hakuwa na matamanio ya kisiasa? Angewezaje kuacha umati mkubwa kama huo bila kauli hata moja ya kisiasa?

Magoha alituacha vinywa wazi alipoondoka wakati tu bendi ya wanamuziki wa ohangla ilipoelekea kuanza burudani. Ilikuwaje kwa mtu ambaye alikuwa mwanachama wa bendi maarufu ya muziki mapema maishani akaondoka bila hata kucheza kidogo? Huyo alikuwa Magoha.

Muda ulikuwa mfupi. Alikuwa na hafla nyingine ya kuhudhuria au kazi za kushughulikia. Utumishi kwa watu ulikuwa aina fulani ya wito mkuu kwa Magoha.

Kisa cha pili kilitokea miaka kadhaa awali alipokuwa Naibu Chansela wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Kulikuwa kumezuka fujo wakati wa uchaguzi wa maafisa wa Chama cha Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi (SONU). Ilidaiwa Babu Owino, aliyekuwa mgombeaji katika uchaguzi huo, alikuwa amepinga baadhi ya matokeo na kusababisha fujo katika kituo kimoja cha kura.

Uchaguzi huo ulifutiliwa mbali na kamati ya muda ikabuniwa ili kuendesha shughuli za SONU. Nilialikwa kwa mkutano katika afisi ya Magoha kujadiliana kuhusu jinsi ya kuunda Kamati ya Muda.

Magoha alifafanua wajibu wa viongozi wa wanafunzi katika chuo kikuu. Lakini alisita katikati na kushangaa ni kwa nini uvumi ulikuwa umeenea chuoni humo eti anamuogopa Babu Owino. Aliangua kicheko, akitwambia "mnitazama vizuri"na kumlinganisha na Babu Owino.

Aliuliza "Kwa nini watu wanasema kuwa Magoha anabeba bunduki kwa sababu ya Babu Owino, kweli?" Kwa nini nimuogope Babu Owino?' Baadaye, Magoha aliishia kufanya kazi na Babu Owino alipochaguliwa Mwenyekiti wa SONU. Kwa upande wake, Babu Owino alikuwa Bungeni Magoha alipofika humo kupigwa msasa baada ya kuteuliwa kuwa Waziri wa Elimu.

Visa hivi viwili vinamuonyesha Magoha kuwa mtu alyekuwa na hakika ya mawazo na vitendo vyake. Katika Chuo Kikuu cha Nairobi, alifuatilia miradi yake kwa makini, akionekana kuwa na nia ya kufanya chuo kikuu hicho kuwa bora zaidi katika eneo hili. Miradi kadhaa ya miundomsingi chuoni humo ni ushahidi wa maono yake.

Jumba la University Tower, katika Chuo Kikuu Cha Nairobi, daima litabakia ukumbusho kwa wengi waliosoma, kufanya kazi na kupitia humo kama ushahidi wa maono ya Magoha kwa taasisi hiyo.

Wenzake chuoni humo walimtaja kuwa mtu aliyetumia kifua alipotaka kitu kifanywe. Lakini walisahihisha kauli hiyo mara moja kwa kutambua jinsi alivyokuwa mtu aliyemsikiliza kila mtu. Wengine wengi walimtaja kuwa aliyekuwa na huruma kwa waliofika afisini mwake kuomba msaada.

Lakini ni wachache sana waliokuwa tayari kukutana naye ana kwa ana au kumkabili katika mkutano. Kimo chake, sauti na macho zilitosha kuzima kauli zozote pinzani.

Watu kama hao wenye kujitolea kwa dhati ni adimu nyakati hizi lakini kumbukumbu zao hubakia kama mabango yanayoelezea maana hasa ya utu.

***Dkt Odhiambo ni mhadhiri mkuu, Idara ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Nairobi. tom.odhiambo@uonbi.ac.ke; odhiambotom@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group "Digital Copy"

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep




**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM